UKURASA WA 4

**Japan** yaipatia Tanzania bilioni 354/- kuendeleza kilimo, wakulima




UKURASA WA 4

**Kampeni** ya msaada kisheria ya Mama Samia kuwafikia wafungwa, mahabusu



UKURASA WA 16

**Wagonjwa** wa kipindupindu jijini Mbeya wafikia 340




# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Januari 15, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581922

Nipashe digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com




LEMA ASEMA...

# Mbowe akishinda, sitagombea ubunge

- **Atangaza** rasmi kumuunga mkono Lissu, adai uchaguzi wa kanda ulikuwa na mchezo mchafu; CCM yatia neno...

*Endelea Ukurasa 2 & 3*



## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### WATAKA UCHAGUZI S/MITAA URUDIWE

WAGOMBEA watatu wa nafasi ya uenyekiti wa Serikali za Vijiji wilayani Mkuranga wamemburuta mahakamani Msimamizi wa Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakidai matokeo hayakuakisi...

UKURASA WA 7

### MAHAKAMA YAMWONYA MTOTO WA MBOWE

## Wilaya tano hatari zaidi kwa matende na mabusha zatangazwa

UKURASA 18

# Lori laua 11 waliokwenda kuwaokoa waliopata ajali

UKURASA 2



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Burian akiwa na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa huo, William Mwamasika, walipotembelea eneo la ajali iliyotokea katika kijiji cha Chang'ombe, Kata ya Segera, wilayani Handeni jana. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

**MICHEZO** **CAF YAFUNGIA MASHABIKI SIMBA** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Lema: Sitagombea ubunge Mbowe akishinda CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya ukimya wa muda mrefu, hatimaye Godbless Lema, amechagua upande wa kuunga mkono katika kinyang`anyiro cha nafasi ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mwenyekiti huyo mstaafu wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini ametangaza rasmi atamuunga mkono Tundu Lissu katika kinyang`anyiro hicho, huku akiwa na lingine la ziada kwamba hatogombea ubunge jimboni Arusha Mjini ikiwa Freeman Mbowe atachaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa chama hicho.

Lema alitangaza hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam.

Desemba 24 mwaka jana, Nipashe ilizungumza na Lema kutaka kujua upande anaounga mkono kati ya vigogo hao wawili wanaogombania nafasi ya uenyekiti wa chama, lakini alisema amejifungia kufanya maombi ili Mungu amwongoze kujua upande upi aunge mkono, akiahidi angetangaza baadaye.

Katika mkutano na waandishi jana, Lema alimshauri Mbowe ajitoe kwenye kinyang'anyiro hicho na kumwachia Lissu huku akimsisitiza asikilize ushauri wa familia yake iliyomwomba apumzike.

Lema alisema anaamini familia ya Mbowe iliongozwa na Mungu kumwambia apumzike na akatoa tahadhari kwamba kuna hatari kubwa mwenyekiti huyo wa sasa wa chama hicho akapoteza heshima yake endapo atang`ang`ania kugombea nafasi hiyo.

"Mimi ushauri wangu kwa mwenyekiti, sikiliza familia yako, imeongozwa na Mwenyezi Mungu kukwambia upumzike. Akipumzika atakuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya chama wa kudumu mpaka siku atakapofariki dunia, maana yake anaendelea kutoa msaada, mawazo," alisema Lema.

"Hiki chama ni mtoto wake, amekuwa nacho, hataacha kianguke, atakuwa kwenye Kamati Kuu ambayo ndiyo inafanya kazi kubwa kwa niaba ya Mkutano Mkuu na Baraza Kuu. Lissu akishindwa itaitishwa kamati itamwondoa," aliongeza.

Lema alisema ni vyema chama kufia kwenye mikono ya mtu mwingine kuliko chama kifie kwa Mbowe.

"Yaani mimi ningekuwa Mwenyekiti (Mbowe), ili kulinda heshima yangu ya miaka 30, kuliko chama kifie kwangu mimi ambaye nimejenga 'legacy' kubwa, nitaruhusu hicho chama kifie kwa mtu mwingine," alisema Lema.

Aliwashangaa wale ambao wanasema bila Mbowe, CHADEMA itakufa, akihoji "Hivi Mwenyekiti (Mbowe) akifa au anaumwa, akashindwa kufanya kazi, chama kitakufa?"

Lema pia alimshauri Mbowe kusikiliza na kuzingatia maoni wa wananchi wanayotoa kupitia mitandao ya kijamii kuhusu nafasi hiyo anayogombania tena.

"Tukipuuza hayo maoni, uchaguzi tukakwenda keshokutwa pale, akashindwa, legacy yake itakufa siku hiyo hiyo. Kutakuwa na shangwe ya kumwangusha mwasisi na mimi ninaona hii ni hatari kwa ndugu yangu," alisisitiza.

Lema alisema anaamini kwamba atakuwa kwenye wakati mgumu kwa kuchagua kuwa upande wa Lissu na kwamba anaamini alichochagua ni demokrasia na si utamaduni.

Lema alisema yupo kiongozi mmoja ndani ya chama hicho ambaye alikwenda mpaka kwa mama yake kumwomba amshauri kuhusu msimamo wake huo.



"Mama yangu anaweza asinielewe, baba yangu anaweza asinielewe. Na kuna mtu mmoja amekwenda hadi kijijini kule akamwambia mama kwamba 'mwambie Lema asimwache kaka yake, maana akishinda, Lema atakuwa kwenye wakati mgumu, anaweza hata akapoteza ile nafasi yake ya kugombania ubunge'," alidai Lema.

Lema alisema hafanyi kazi ya siasa ili kuwa kiongozi bali kwa sababu ana wito wa kufanya kazi hiyo kwa ajili ya wajukuu wa nchi hii waje wawe na maisha mazuri.

"Haya maisha ni mafupi sana, yaani pilika zote hizi... ninakwenda jela, ninakimbiza familia, ili tu eti nije kuwa mbunge! Hebu jamani tusidhalilishane, sitagombania ubunge Arusha Mjini mwaka 2025 halafu nitaendelea kuwa mwanaharakati huru.

"Kwa hiyo nitamuunga mkono Lissu na Mwenyekiti (Mbowe) akishinda sitagombania ubunge Arusha Mjini," alisisitiza Lema.

Alisema atakuwa tayari kumuunga mkono na kumsaidia kumpigia kampeni atakayegombea kwenye jimbo hilo kupitia chama chao hicho, hata kutumia rasilimali zake.

Lema pia alisema: "Hata yakiitishwa maandamano ya kudai Katiba Mpya na tume huru nitakuwa mbele, na nikigundua kuwa mimi kuwa mwanachama wa chama hiki ni kero kwao, nitakuwa mwanaharakati huru, lakini kamwe sitafanya kazi ya CCM (Chama Cha Mapinduzi)."

Lema pia alisema atakuwa tayari kurudi tena kwenye vyombo vya habari kupambana na wapambe wa Mbowe endapo watatoka hadharani na kuanza kumshambulia baada ya kuweka msimamo wake huo.

"Mbowe ni kaka yangu, tunafahamiana, ananijua na mimi ninamjua vizuri sana, niwaonye wapambe msinifanye niitishe mkutano mwingine na waandishi wa habari, chukulieni kama hili ni tendo langu la kidemokrasia na mimi huwa ninaongozwa na Mungu. Msinitukane, msinidhalilishe kwa sababu ninamuunga mkono Lissu.

"Mkifanya hivyo mimi ninaweza kuamua kuja kujibu, tutagombana na ndugu yangu... nisaidieni mimi na ndugu yangu tukikutana Machame Krismasi tushikane mkono," alisema Lema.

Lema alisema anaamini kwa msimamo wake huo, hata familia yake haitafurahia.

Aliwaomba wajumbe kutoka Kanda zote kumpigia kura Lissu na kuepuka kushawishiwa kwa namna yoyote.

"Wajumbe ni hatari sana, ninataka niwaambie hivi, ukiona kuna mtu anataka kununua uongozi ambao hana mshahara, huwa kuna mahali analipwa mshahara kwa ajili ya huo uongozi na wajumbe mkikubali kupewa pesa, mkapiga kura kwa ushawishi wa pesa, jambo la msingi ni sahihi CCM kuendelea kutawala nchi hii?

"Kama wajumbe wa CHADEMA, wanaweza kupiga kura ya nguvu ya pesa na siyo utashi na uelewa, tuna tatizo kubwa kama nchi. Chama cha siasa cha upinzani mnatakiwa kuwa na aina ya viongozi ambao akiona bunduki anaifuata anasema moyoni hata nikifa, ninakufa kwa sababu ninapigania kweli," alisema Lema.

Lema pia alitumia mkutano huo kutangaza kumuunga mkono John Heche katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti anayogombea, akisisitiza kuwa:

"Mimi ningekuwa na mamlaka ya kichama, Wenje (Ezekiel - anayechuana na Heche), hakutakiwa kuwa mwanachama wa CHADEMA leo."

Lema pia alisema kuwa Lissu akishinda, watamwomba msamaha Dk. Wilbroad Slaa na watamrejesha kuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho.

"Ushauri wangu kwa kaka yangu Freeman Mbowe, msaidie Lissu kuwa mwenyekiti, kama una shaka na uongozi wake, utakuwa mjumbe wa Kamati Kuu, sina kinyongo na wewe kaka yangu... tukikutana Machame tusalimiane lakini ikiwa itashindikana kusalimiama kwa sababu ya msimamo huu mimi sitajali sana, nitaendelea na maisha yangu kama kawaida," alisema.

Lema alidai kukataa kwake kugombea tena nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini ni baada ya kugundua kulikuwa na mpango uliosukwa ili kuwaondoa katika mfumo wa uongozi ndani ya chama hicho.

Alidai walengwa wakuu katika mpango huo ni yeye, Heche, Peter Msigwa na Lissu.

***Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz***

# Lori lilivyoua 11 waliokuwa wanawaokoa waliopata ajali

**Na Oscar Assenga,** HANDENI

NI simulizi iliyojaa simanzi na vilio. Wananchi walijitokeza kutoa msaada wa haraka wa kuwaokoa majeruhi wa ajali, wanapoteza maisha kwa kuparamiwa na lori lenye shehena ya saruji lililopoteza mwelekeo.

Ni mkasa uliogharimu maisha ya watu 11 huku wengine 12 wakiwa majeruhi baada ya kukanyagwa na lori aina ya VOLVO lenye namba za usajili T 782 BTU lililokuwa linatokea Tanga kwenda Arusha.

Imeelezwa kuwa lori hilo lilipata hitilafu katika mfumo wa breki kisha kupoteza mwelekeo na kuwagonga watu hao eneo la Chang'ombe, Kata ya Segera, Wilaya ya Handeni.

Akieleza jana chanzo cha ajali hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Almachius Mchunguzi alisema ajali hiyo ya VOLVO ilitokea saa 3:30 usiku wa Januari 13 mwaka huu na kusababisha vifo vya watu hao.

Kwa mujibu wa ACP Muchunguzi, ajali hiyo ilitokea baada ya VOLVO kuwagonga watu waliokuwa wanashangaa ajali nyingine ya basi la abiria, namba T 720 EJP aina ya TATA, lililokuwa limeteleza na kuacha barabara bila kusababisha madhara yoyote kwa binadamu.

"Jeshi la Polisi linamsaka dereva aliyejulikana kwa jina la Baraka Meleckdezeck, maarufu Urio, aliyekuwa anaendesha VOLVO kutokana na kugonga watu waliokuwa pembeni mwa barabara wakiangalia ajali iliyokuwa imetokea katika eneo la Chang'ombe.

"Gari namba T 720 EJP aina ya TATA basi, lilikuwa limeteleza na kuacha barabara bila kusababisha madhara yoyote kwa binadamu," alisema.

Waliofariki dunia na kutambuliwa katika ajali hiyo ni Hamisi Mkumbuka (Saa Mbovu), Bujaga Rashid, Adamu Maneno (Mkweguto), wote wakazi wa Maili Kumi, wilayani Handeni.

Wengine ni Sawebu Juma (Kashaija), mkazi wa Dar es Salaam, Joseph Mboye, Nasib Shemsanga, Twalib Kashaija, Ignatus Shayo, Rashid Yahaya, Salim Abdurahaman na mwingine ambaye mwili wake haujatambuliwa.

Kwa mujibu wa Kamanda Muchunguzi, majeruhi 12 wamepelekwa Hospitali ya Magunga, wilayani Korogwe kwa ajili ya matibabu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Magunga, Dk. Miriam Cheche, alisema wamepokea majeruhi wa ajali hiyo; wanne wamehamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo) na watatu wamefariki wakiwa wanapatiwa matibabu.

Alisema hospitalini huko kuwa wamebakiwa na majeruhi saba ambao wanaendelea na matibabu.

**MAJERUHI ALONGA**

Mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo, Faraji Karata alisema kuwa aliposikia ajali hiyo, alikimbia kwenda kutoa msaada kwa majeruhi na kuimarisha ulinzi, lakini alijikuta akipatwa na ajali.

"Wakati lori hilo la VOLVO linakuja tuliliona, lakini hatukuelewa ilikuwaje likatufikia na kuua wenzetu na sisi kujeruhiwa. Ninashukuru Mungu kwa kuniokoa, sasa hivi ninaendelea na matibabu," alisema Karata.

SERIKALI YABEBA MSIBA

Mkuu wa Mkoa huo, Balozi Dk. Batilda Buriani, alisema jana kuwa serikali itabeba gharama za maziko ya watu hao pamoja na matibabu ya majeruhi 12.

"Serikali itagharamia matibabu kwa wale wote walioathirika na ajali hii na itagharamia usafiri kwa waliofariki dunia. Tunatoa ubani kwa wale wote waliofiwa na jamaa zao na kuwapa sanda na kuwasitiri," alisema.

HABARI KITAIFA

# CCM yatia neno uchaguzi CHADEMA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema hakihusiki kwa namna yoyote au jambo lolote na uchaguzi mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuwa kina mambo mengi ya msingi ya kufanya.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makala, alisema hayo jana wakati akizungumza na moja ya vyombo vya habari kuhusu maandalizi ya Mkutano Mkuu wa CCM, utakaofanyika mwishoni mwa wiki hii.

Makala alisema hayo wakati akijibu swali la mwandishi aliyehoji kuwa CCM inazungumziaje maneno ambayo yamekuwa yakisemwa na baadhi ya watu kuwa inahusika na kuchochea mvutano uliopo hivi sasa ndani ya chama hicho kikuu cha upinzani.

"Nitumie nafasi hii kama msemaji wa chama kwamba CCM haikusiki na jambo lolote na uchaguzi wa CHADEMA. CCM tunayo majukumu mengi ya kufanya na viongozi wote na watendaji mawazo yetu yote, akili zetu na nguvu zetu zote tumezielekeza kwenye mkutano mkuu huu maalum. Hatuwezi kuhangaikia kujihusisha na kazi za chama kingine. Kwanza tunajihusisha kwa tija ipi na kwa faida ipi?

"Kwa hiyo mimi niseme tu kwamba hayo ni maneno ambayo wanasema wao wenyewe kambi zao hizo zinachafuana. Kwa hiyo ndiyo mambo ambayo nimejifunza kwamba kuna hela chafu kuna mnyukano ni jambo ambalo najifunza ndani ya chama hicho ambako uchaguzi unaendelea. Kwa hiyo CCM isihusishwe na jambo lolote. Tuna mambo mengi ya msingi ya kufanya," alisisitiza.

Makala pia alisema anakitakia uchaguzi mwema chama hicho, kipite salama katika mnyukano huo mkali na kuwapata viongozi wengine watakaokiongoza.

"Tunawatakia kila la heri kwa maana tunayasikia mengi na sisi tunawaombea wavuke salama kwani CCM inahitaji upinzani wenye nguvu na tunatumaini kuwa watatoka salama kwenye mnyukano huu na kuwapata viongozi wao," alisema.

Pia alisema mikutano hiyo miwili (CCM na CHADEMA) ina utofauti mkubwa kuilinganisha kwa kuwa wa CCM ni wa watu wenye furaha huku CHADEMA wakiwa wa mtifuano.

"CCM kwa kweli tumejipanga ni mkutano wa aina yake. Tuna viongozi, mabalozi, wageni wajumbe 1,950 na waalikwa zaidi ya 3,500. Hivyo kwa kigezo cha kujifunza ni kwamba CCM haina la kujifunza kwa CHADEMA kwa kuwa mkutano wetu ni wa aina yake," alisema.

Makala alisema maandalizi ya mkutano mkuu maalum wa kihistoria wa chama wenye ajenda kuu tatu, yamekamilika.

Alisema mkutano huo utakuwa na kazi ya kujaza nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama, kupokea taarifa za utekelezaji Ilani kwa serikali mbili ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, na kupokea taarifa ya kazi za chama katika kipindi cha 2022/2025.

"Maandalizi kwa kiasi kikubwa yamekamilika, Dodoma kumekucha tunawakaribisha wajumbe wote wa mkutano mkuu na waalikwa kuja," alisema.

Kuhusu mchakato wa kumpata Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, alisema hiyo ni nafasi ya juu na kwamba ni msaidizi wa juu wa mwenyekiti wa chama, hivyo wanakuwapo wawili Bara na Zanzibar.



"Kama unavyofahamu nafasi hii ilikuwa wazi baada ya (Abdulrahman) Kinana kuomba kupumzika. Umefika wakati mwafaka wa kujaza nafasi hiyo, hivyo utaratibu ni kwamba nafasi hii haigombewi, hujazi fomu, haina kinyang'anyiro. Inaanzia mchakato wake katika Kamati Kuu kufikiria na kutoa mapendekezo ya mtu anayefaa kujaza nafasi hiyo," alisema.

Baada ya hapo, alisema jina litapelekwa NEC ambayo ikiridhia na kupitisha, jina hilo litapelekwa kwenye Mkutano Mkuu ili wajumbe wapige kura za ndiyo na Hapana. Huo ndio mchakato wa kumpata Makamu Mwenyekiti," alibainisha.




# Kasi matumizi ya baruti yazidi kutisha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MATUMIZI ya baruti nchini yameongezeka kutoka wastani wa tani 3,000 kwa mwaka katika miaka ya 1990 hadi kufikia tani 26,516.07 kwa mwaka jana, imeelezwa.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Ramadhani Lwamo, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati akifungua kikao cha kuwajengea uwezo wakaguzi wa migodi na baruti nchini.

Lwamo alisema kuongezeka kwa matumizi hayo kunachangiwa na uchimbaji madini, utafiti wa mafuta, gesi asilia na ujenzi wa miundombinu nchini.

Alisema kuongezeka kwa matumizi hayo kumesaidia kupaa kwa biashara ya baruti nchini tofauti na miaka ya nyuma.

"Matumizi makubwa ya baruti maana yake uchimbaji umeongezeka, hivyo bila udhibiti italeta madhara. Kikao hiki ni kujengeana uwezo lengo kuhakikisha wachimbaji hawapotezi maisha au viungo kwa ajili ya matumizi ya baruti.

"Udhibiti madhubuti ni muhimu, mkadhibiti katika maeneo yenu, itakuwa ni aibu mkaguzi mgodi na baruti eneo lake mtu akapata madhara," alisema.

Lwamo alisema hadi sasa kuna zaidi ya bohari (magazine) 231, stoo 493, masanduku ya kuhifadhia baruti 279 yaliyosajiliwa kwa ajili ya matumizi migodini na maeneo ya biashara.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Ukaguzi Migodi na Mazingira nchini, Hamisi Kamando, alisema kumekuwa na matukio ya ajali yanayotokana na kukiuka Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963, Kanuni za Baruti za Mwaka 1964 na taratibu zingine za usimamizi wa baruti.

Mwanasheria Damian Kaseko aliwataka wakaguzi migodi na baruti kusimamia sheria, kanuni na sera ili kuepusha migogoro na kuwa na mipaka katika utekelezaji wa shughuli zao.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba na Balozi wa Japan nchini anayemaliza muda wake, Yasushi Misawa, wakitiliana saini hati ya mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Ubalozi wa Japan, katika Ofisi Ndogo za Hazina, jijini Dar es Salaam jana, ambapo alitiliana saini mkataba mwingine wa mkopo wenye masharti nafuu kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) wa Yen za Japan bilioni 22.742 (sawa na sh. bilioni 354.45), kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Kilimo Vijijini. **PICHA: WF**

# Kampeni ya msaada kisheria ya Mama Samia kuwafikia wafungwa, mahabusu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inatarajiwa kuanza kwenye mikoa sita na itapita kwenye Magereza mbalimbali nchini kuonana na wafungwa na mahabusu kuwapa msaada huo wa kisheria.

Mratibu wa Kampeni hiyo kitaifa katika Wizara ya Katiba na Sheria, Esther Msambazi, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye mafunzo ya siku mbili ya waratibu wa ngazi ya halmashauri ambao watasimamia utekelezaji wa kampeni hiyo.

Alisema waratibu hao wana jukumu la kuhakikisha wanaratibu vyema kampeni hiyo kwa kuhakikisha wananchi wengi wanafikiwa kupata msaada wa sheria.

Msambazi alisema kampeni hiyo imeshafanyika kwenye mikoa 11 na imebaki mikoa 15 na kwamba kwa mwezi huu wanatarajia kwenda kutekeleza kampeni hiyo kwenye mikoa sita.

"Lengo ni kuwafikia wananchi wengi kwa wakati mmoja na kuhakikisha tunagusa maeneo na mikoa yetu na leo hii tuko hapa na wataalamu wengi kuhakikisha tunakuwa na uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa kampeni hii.

"Tuko hapa leo kwaajili ya kukubaliana kwamba hiki tunachofanya Wizara ya Sheria ndiyo malengo yetu wadau wote na tuko na mawakili 20 kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa hati ya makubaliano tuliyoingia Desemba, 2024 kuhusu kushirikiana kwenye eneo la msaada wa kisheria," alisema.

Alisema kampeni hiyo inayohusisha wadau mbalimbali inatarajiwa kuanza tarehe 24 mwezi huu wakianzia mikoa ya Lindi, Mtwara, Kigoma, Geita, Katavi na Kagera.

"Baada ya mafunzo haya waratibu hawa wa halmashauri kwa kushirikiana na waratibu wao wa mikoa wataondoka kwenda kujipanga kwaajili ya kuanza utekelezaji wa kampeni hii mara moja," alisema.

Alisema ushiriki wa TLS ni muhimu sana kwani mawakili wa taasisi hiyo wanaoshiriki kwenye kampeni hiyo wanatoa msaada wa sheria kwa wananchi kujua wajibu na haki zao.

Alisema kuna wananchi wenye migogoro mbalimbali lakini wanakosa wanasheria wa kuwasimamia hivyo ushiriki wa TLS utasaidia kuongeza tija kwenye kampeni hiyo.

"Wananchi wenye mashauri mahakamani na wanaotarajiwa kuwa na mashauri mahakamani ni wengi sana sasa wanaenda kupata uwakilishi wa mawakili bila shaka yoyote," alisema

Alisema kwenye kampeni hiyo, watawajengea uwezo mawakili nchi nzima ambapo watakuwa na mawakili wawili kila halmashauri ambao watatoa huduma za msaada wa kisheria ikiwa ni sehemu ya makubaliano na TLS na wadau wengine wa ngazi tofauti tofauti.

Akitoa hotuba ya kuuanza mwaka mpya, Rais Samia Suluhu Hassan aliahidi kuwa serikali itafanya marekebisho ya sheria mbalimbali zinazohusu haki jinai na kutoa msaada wa kisheria kwa wasio na uwezo.

## Japan yaipatia Tanzania bil. 354/- za kuendeleza kilimo

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI ya Japan imepatia Tanzania mkopo nafuu wa Sh. bilioni 354.45 kwa ajili ya utekelezaji mradi wa uendelezaji kilimo vijijini.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam jana baada ya kutiwa saini kwa mkataba huo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alisema mradi huo utatekelezwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ukisimamiwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA).

Alisema utekelezaji mradi huu utachochea ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kuongeza uzalishaji kwa wakulima kupitia upatikanaji wa mitaji nafuu.

"Hii itafikiwa kwa kutoa mikopo ya muda wa kati na mrefu kwa wakulima, vikundi vya uzalishaji na taasisi zinazojihusisha na kilimo kwa kuziwezesha kuwekeza katika kilimo cha kisasa, kupata pembejeo bora na teknolojia ya juu ya kilimo," alisema Dk. Mwigulu.

Alisema msaada huo utachochea upatikanaji mitaji ya kilimo, wakulima kuwa na mazao mchanganyiko na kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi, ambako kutachangia usalama wa chakula, maendeleo vijijini na uimara wa uchumi kwa ujumla.

Alisema Tanzania imenufaika na ufadhili wa Japan kwa miaka zaidi ya 60 hasa kwenye sekta za kilimo, maji, afya, nishati, usafirishaji na elimu kupitia kujengewa uwezo.

Pia alisema Tanzania imeendelea kunufaika na ufadhili unaotolewa kupitia mashirika makubwa ya kimataifa ambako Serikali ya Japan inachangia kwa ajili ya miradi mingine ya kijamii na kiuchumi.

Alisema msaada huo unaendana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao una maudhui ya kufikia ushindani na uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya watu ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Vilevile, alisema msaada huo unaendana na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambao unalenga kuimarisha na kuchochea matumizi ya zana za kisasa za kilimo, usalama wa chakula na lishe, kuwezesha upatikanaji wa masoko na kuwezesha uongezaji wa thamani.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Japan, Fujii Hisayuki alisema ushirikiano wa Japan na Tanzania ni wa muda mrefu na umejielekeza katika sekta muhimu.

Alisema sekta ya kilimo Tanzania imekuwa muhimu kwa uchumi kwa sababu imebeba asilimia kubwa ya wananchi ambao wengi wao wamejiajiri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Mandeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, alisema tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani amekuwa ikiipa kipaumbele sekta ya kilimo ikiwamo kuongeza bajeti.

Alisema kwa miaka aliyokuwa madarakani (Rais Samia) ameipatia TADB zaidi ya Sh. bilioni 954 kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kupitia mikopo nafuu.

TANGAZO

# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

UCB CARING FOR FAMILY ECONOMY

## GHARAMA ZA HUDUMA KUFIKIA TAREHE 31.12.2024

| A | DEPOSIT RATES | Descriptions | RATES(USD) - Products | RATES(TZS) - Products |
|---|---|---|---|---|
| | Mavuno Account - Special Deposit Account (p.a) | | | 9% |
| | **Fixed Deposit** | | | |
| | 3 Months | | | 4% |
| | 6months | | | 5% |
| | 12Months | | | 6% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 50Mil | | | 6% to 7% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 100Mil | | | 8% to 9% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 500Mil | | | 10% |
| B | **CHARGES AND FEES** | | | |
| | **ITEM/TRANSACTION** | | | **CHARGE/FEE** |
| 1 | **Current Accounts** | | | |
| | Minimum Opening balance - Company and individual | | 50.00 | 100,000.00 |
| | Minimum Operating Balance | | | - |
| | Monthly Statement enquiry | | 2.00 | TZS 1,500 per month and TZS 700 for extra page |
| | Monthly Ledger fee | | 5.00 | 15,000.00 |
| | Account closing charges | | 10.00 | 20,000.00 |
| | Sale of bankers cheque | | | 30,000.00 |
| | Cancelation of bankers cheque | | | 30,000.00 |
| | Cheque book per leaf | | 0.18 | 400.00 |
| | Stop payment order | | 10.00 | 30,000 reported lost/stolen cheque book/leaf (per notice) |
| | Standing order within the bank per entry | | 2.00 | 2,000.00 |
| | Standing order to other banks per entry | | 20.00 | 15,000.00 |
| | Confirmation of Balance and Audit statement | | 25.00 | 50,000.00 |
| | Salary processing fee per entry | | N/A | 2,000.00 |
| | Upaid cheque (RD) | | 40 | 40,000.00 |
| | Montly fees - Parishes Account | | N/A | 5,000.00 |
| | - Other Current Account | | N/A | 15,000.00 |
| | Quartely fees - Other Current account | | 5 | 2,000.00 |
| | Current Accounts - Individual withdrawal over counter | | 5 | 2,000.00 |
| | Current Accounts - Individual monthly fees | | 5 | 5,000.00 |
| | Current Accounts - SACCOS withdrawal over counter | | | 2,000.00 |
| | Deposit fee | | | free |
| | Withdrawal on current account using cheque | | | |
| | | 1 - 399,999 | | 1,500.00 |
| | | 400,000 - 4,999,999 | | 1,800.00 |
| | | 5,000,0000 - 9,999,999 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 and above | | 0.05% |
| | Withdrawal on current account without cheque | Any Amount | | 5,000.00 |
| 2 | **Savings Accounts** | | | |
| | Minimum Operating Balance | Mavuno Saving Account | | 5,000.00 |
| | | Personal Saving | 10 | 10,000.00 |
| | | Other Savings Products | | 10,000.00 |
| | Account closure | | 10 | 20,000.00 |
| | Dormant account reactivation | | 1% of the withdraw amount | free |
| | Withdrawal fee over the counter- Savings Products | | | |
| | | 1 - 399,999 | | 1,500.00 |
| | | 400,000 - 4,999,999 | | 1,800.00 |
| | | 5,000,0000 - 9,999,999 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 and above | | 0.05% |
| | Account maintenance fee - Monthly - Saving products | | | 1,500.00 |
| | - Quartely - Saving products | | | 1,600.00 |
| | Bulk Cash deposit | | | free |
| | New ATM card issuance | | N/A | 10,000.00 |
| | ATM card renewal or replacement | | N/A | 15,000.00 |
| | ATM withdrawal fee | 1,000 - 99,999 | | 1,500.00 |
| | | 100,000 - 400,000 | | 1,700.00 |
| | PIN Reset ATM | | | 5,000.00 |

| 3 | **Electronic Banking** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | SWIFT/TISS transfer | 1 - 10,000,000 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 - 50,000,000 | | 5,000.00 |
| | | 50,000,000 and above | | 10,000.00 |
| | Mobile banking balance enquiry | | | 300.00 |
| | Transfer from bank account to mobile - As per TIPS schedule below | | | |
| | Mobile - PIN reset | | | 2,000.00 |
| | **Other Charges** | | | |
| | Cheque clearing fee (Outward Cheques) | | | 1,000.00 |
| | EFT | | | 2,000.00 |
| | Search fees (including vouchers) | one Month | | Free |
| | | Two(2) to six(6) month | 10 | 20,000 |
| | | Above six(6) month | 25 | 50,000 |
| | | CCTV footage Maximamu of 3 months | Tzs equivalent | 30,000 |
| | | | | |
| | Uncollected cheque book (after notification) | | | TZS 2,000 per month |
| | Coins deposit | Percentage of deposit amount for non parish | | 3% |
| | Brela Search Fees | Company Limited | | TZS 25,000 |
| | | Trade name | | TZS 7,000 |
| 4 | **Internet Banking** | | | |
| | 24/7 Transfer UCB to UCB | | | Free |
| | 24/7 Transfer (Other Banks) | | | AS PER TIPS AND TISS SCHEDULE |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) - as per TIPS schedule below | | | |
| | 24/7 Airtime processing | | | free |
| | 24/7 Government payment | | | free |
| | 24/7 Other payments (utility) | DSTV, Star Times, AZAM, Subsciption services, bettings, Air tickets etc. | | 1,500.00 |
| | Balance inquiry | | | Free |
| | Monthly fee per retail user | | | 1,500.00 |
| | Monthly fee for corporate user | | | 2,500.00 |
| | Retail & Corporate subsricption | | | Free |
| | Bank statement self download | | | 500.00 |
| | Cheque book request 100 leaves | | | 47,200.00 |
| | Cheque book request 50 leaves | | | 23,600.00 |
| | PIN Regeneration | | | Free |
| | Salary processing | | | 500.00 |
| | Standing Order Instructions | | | 2,000.00 |
| 5 | **TIPS** | 1 - 50,000 | N/A | 500.00 |
| | | 50,000 - 500,000 | N/A | 1,000.00 |
| | | 500,000 - 5,000,000 | N/A | 1,500.00 |
| | | 5,000,000 - 20,000,000 | N/A | 2,000.00 |
| 6 | **Agency Banking** | | | |
| | Agent Cash withdraw charges | 1,000-99,999 | N/A | 1,700.00 |
| | | 100,000-299,999 | N/A | 1,800.00 |
| | | 300,000-999,999 | N/A | 3,250.00 |
| | | 1,000,000-1,999,999 | N/A | 5,450.00 |
| | | 2,000,000-2,999,999 | N/A | 6,550.00 |
| | | 3,000,000-5,000,000 | N/A | 10,000.00 |
| | | 5,000,001-10,000,000 | N/A | 12,000.00 |
| | Agent cash deposit | | | Free |
| | Agency Banking Inquiry | | | 500.00 |
| | Agency Mini-Statement | | | 500.00 |

UCB CARING FOR FAMILY ECONOMY

**UCB OFFERS THE FOLLOWING PRODUCTS:**

- *Savings Accounts*
- *Current Account*
- *Elimu Juniour Account*
- *Mavuno Savings Account*
- *Uchumi Savings Account*
- *Fixed Deposit Accounts-(FDR) with attractive Rates*
- *Forex Accounts*
- *Bureau De Change*
- *ATMs Services,all over the Country-Umoja Switch*

218324902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kambi upimaji afya ziwe endelevu kusaidia wasiojiweza

**UTARATIBU** wa kuanzisha kambi maalumu zinazosaidia wananchi wasioweza kumudu gharama, kupima afya umesaidia kugundua magonjwa mengi na kutoa fursa ya kusaidiwa matibabu.

Utaratibu huu umesaidia wananchi wengi kugundua maradhi ambayo walikuwa hawajui kama wanayo na hatimaye kupatiwa tiba.

Kuna watu wanatembea na maradhi ambayo sio rahisi kuyagundua mpaka utakapokwenda kwa wataalamu kupimwa.

Wakati Waziri wa Afya akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya bajeti ya wizara yake bungeni, alisema serikali inakusudia kuja na chombo muhimu kitakachokuwa kinadhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi.

Afya ni muhimu katika maisha ya binadamu hivyo ni lazima suala la gharama liangaliwe ili lisiwaumize wananchi hasa wasiokuwa na uwezo.

Kwa kuanzishwa chombo chenye uwezo wa kusimamia na kudhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi hususan wasio na bima ya afya, malalamiko yatapungua.

Utaratibu huu utasaidia kudhibiti utozaji gharama holela unaofanywa na baadhi ya madaktari katika hospitali za binafsi na zile za serikali ili kuwapa unafuu wananchi.

Vyombo kama hivi vimefanikiwa pia katika huduma za mafuta ya petroli ambapo inafahamika kila mtu anapokwenda kwenye kituo cha mafuta kujaza kwenye gari yake anakuta bei elekezi.

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagonjwa wanapokwenda kutibiwa kukuta wakitozwa gharama kubwa kumuona daktari kabla ya kupata matibabu, hali inayowafanya wasiokuwa na bima za afya kushindwa kulipia na kuamua kwenda kujaribu tiba zingine mbadala.

Kwa mujibu wa wasilisho la makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Fedha, kwenye vitita vya NHIF, madaktari bingwa katika ngazi ya rufani mkoa, ada imeongezeka kutoka Sh. 15,000 hadi 25,000 ambayo ni sawa na kumuona daktari aliyepo ngazi ya kanda na taifa.

Kiwango hiki cha kumuona daktari kinatoa hamasa kwa madaktari hao kufanyakazi katika mazingira yoyote watakayopangiwa, ikiwamo pembezoni.

Aidha, ada ya usajili na kumuona daktari kwa wanufaika wa NHIF kwa ngazi ya wilaya imeongezeka kutoka Sh. 2,000 hadi Sh. 7,000 kwa ngazi ya zahanati ada imeongezeka kutoka Sh. 1,000 mpaka Sh. 3,000.

Aidha, kitita hicho kitaboresha upatikanaji wa huduma bora za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wanachama.

Pia, kimezingatia maendeleo ya teknolojia ya tiba, hali halisi ya bei katika soko na uwezo wa mfuko kugharamia huduma hizo huku ukiendelea kuwa endelevu kwa kuzingatia ushauri wa taifa, mapendekezo ya tathmini ya uhai na uendelevu.

Wizara ya Afya pia imetaja vipaumbele na kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa na kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa.

Katika bajeti hiyo wizara imetenga Sh. bilioni 117.61 kuimarisha huduma ya kinga dhidi ya magonjwa ikiwamo kuimarisha utekelezaji wa afua za chanjo kwa kuwafikia watoto 3,117,564 wenye umri chini ya miaka miwili, wasichana 871,429 wenye umri wa miaka tisa na wajawazito 3,298.437.

Kwa mujibu wa waziri, Sh. bilioni 17.18 zimetengwa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, ikiwamo kujenga, kukarabati na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga wagonjwa waliozaliwa na uzito upungufu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Shule zinapoanza, anza na usalama

**SHULE** za msingi na sekondari zimefunguliwa wiki hii hivyo suala la watoto kusoma, kufurahia shule katika miundombinu bora pamoja na kufaulu ni kipaumbele, lakini usalama wa watoto na ulinzi wao ni jambo linalohitaji wazazi, walezi na jamii kulipa umuhimu wa kipekee.

Kumbukeni pia kuwajali na kuwalinda zaidi wenye mahitaji maalumu wasiona, wasiosikia, wenye ualbino na ulemavu mbalimbali wa viungo.

Ulinzi na usalama unagusa kila mmoja kuwaangalia kuanzia shuleni wanaposoma, mitaani wanapokaa na mambo muhimu wanayohitaji ili kuwasaidia wasome salama, wasinyanyaswe kijinsia hata kuuliwa.

Lakini juhudi hizi ziende pamoja na kuziweka huduma za kijamii kama maji, chakula na mabweni shuleni maana vitu hivyo vinapokosekana huleta shida hasa kwa mabinti ambao wanatumbukizwa kwenye mitego na kukwama kimasomo.

Ni kwa sababu watoto wengi wanaoathirika na ukatili wa kijinsia hasa mabinti kupewa mimba utotoni, kutumiwa kingono na walimu au walezi na hata kuozwa kunaweza kuchangiwa na ukosefu wa huduma za jamii.

Ukiangalia zaidi eneo la sekondari, huduma muhimu zinazozungumziwa hapa ni kama chakula, mabweni, maji, hospitali na usafiri.

Kwa kiasi fulani ukosefu wa bweni huwalazimisha wasichana kupanga nyumba mitaani, wakati mwingine kuishi bila maji kunachangia kujihimu alfajiri kwenda kisimani au mtoni au usiku wa manane kusaka maji yote yakiwatumbukiza kwenye mikono ya wanyanyasaji.

Kusoma pasipo na chakula kunamaanisha njaa isiyovumilika, matokeo yake ni binti kufanya lolote bila kujali itakuwaje ili apate chakula, asife njaa.

Yote hayo na mengine mengi huchangia mimba, utoro na watoto kuchukia shule, kuteswa na kumaliza shule bila kujua kusoma wala kuandika.

Ni vyema wazazi, walezi na wadau wa elimu watatue matatizo hayo yanayohusiana na huduma za msingi ili kupunguza tatizo linalohusiana na kukwamishwa kusoma kutokana na matatizo hayo kila mwaka.

Usalama na ulinzi wa watoto unakwenda mbali zaidi kwa kuwasimamia na kuwaepusha na athari za utandawazi ni kwa sababu umewaharibu watoto wa sekondari na msingi kwa vile wamekuwa wateja wa mitandaoni kujifunza 'maovu.'

Wanatumia simu kuangalia picha kwenye YouTube zenye maudhui ya ngono, kujifunza masuala mengine makubwa kuliko mri wao, wapo wanaojifunza na kufanya uhalifu.

Utandawazi unawatumbukiza katika kupenda muziki wa disko usiku, lakini wale wanaokaa mbali na nyumbani au waliopanga mitaani ni wapenzi wa mikesha ya harusi na ngoma.

Wakati mwingine ni waraibu wa sinema zinazoonyeshwa kwenye mabanda mitaani kama yanavyojulikana kama vibanda umiza.

Wapo wanaocheza kamari, kunywa pombe, kwenda kwenye vijiwe zinapouzwa na kuvutwa bangi. Afya yao kwenye elimu inaporomoka na huenda wakaghadhabika siku ya mtihani wa kuhitimu na kuanza kuandika matusi na kuchora picha za ajabu.

Watoto hawa wanapokosa uangalizi wanaweza kuishi kwenye nyumba za sinema mchana au vibanda umiza, mabinti wanaweza kuzamia kwenye mikesha au wakaranda mitaani kwa maelezo kuwa hakuna mabweni shuleni wanalazimika kupanga.

Wengi huishia kushawishiwa na kutumbukia kwenye vitendo vya kuwakwamisha kimasomo.

Watoto wanaingia mitegoni wanapokwenda kwenye mabanda yanakoonyeshwa video mchana na kukutana na watu wanaowalipia kiingilio, kuwapa chips na soda kitakachofuata ni ulaghai na hadaa za ngono, zinazoweza kuwaondoa shuleni, kupata mimba na kuzitoa utotoni na kuambukizwa magonjwa.

Pamoja udanganyifu huo mabinti wanaweza kuingizwa mtegoni na walimu ambao ama kwa kisingizio cha kuwafundisha twisheni au kuwaomba wasaidie kazi za nyumbani wanawabaka au kuwashawishi kuingia kwenye ngono.

Ni vyema kuwaangalia watoto wasiwe waathirika wa kutafuta fedha za kujikimu kwa kulazimishwa kufanyakazi za kuosha vyombo, kutafuta kuni, kufua nyumbani kwa walimu na wanavijiji au wanajamii ili kupata fedha za kuishi na kununua mahitaji ya msingi ya kitaalamu na maisha.

Wazazi, walezi, jamii na asasi za kiraia waanze kufuatilia na kuhoji sababu za wasichana au wanafunzi kuzurura, kufanya mambo yanayokwenda kinyume na taratibu.

Mambo yasiishe hapo taarifa zifikishwe polisi, dawati la jinsia, kwa watendaji wa elimu na hata viongozi wa siasa ili kupata ufumbuzi.

Jamii isikae kimya maana kudhalilisha watoto hakuwezi kukoma kama jamii itaendelea kunyamaza.

## Mahakama yamwonya mtoto wa Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Kazi imemwonya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe kwa kutofika mahakamani tangu shauri la madai ya malimbikizo ya mishahara ya waandishi wa habari 10 lilipofunguliwa na imemwamuru kulipa fedha hizo.

Dudley ambaye ni mtoto wa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe alipewa amri hiyo jana mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Mary Mrio wakati shauri hilo la madai lilipokuwa linatajwa.

Msajili Mrio alisema shauri hilo liliitwa jana kwa ajili ya kuangalia maombi ya waandishi wa habari ya kumkamata Dudley kuwa mfungwa wa kiraia kwa kushindwa kulipa malimbikizo ya mishahara yao.

Alisema maombi hayo hayajawasilishwa, hivyo aliamuru ndani ya siku saba yawe yamewasilishwa mahakamani kwa ajili ya kupangiwa Jaji wa kuyasikiliza.

Akijibu hoja hiyo, Wakili wa Dudley, Samadani Mngumi alidai hajazungumza na mteja wake zaidi ya kupokea maelekezo ya kufika mahakamani kuomba udhuru hadi Januari 28 aweze kufika.

Msajili Mrio alihoji kwamba anafika mahakamani kulipa au mazungumzo tu na kwamba tangu shauri hilo liwapo hajawahi kuhudhuria.

"Mteja wako ameitwa mara kadhaa, hajawahi kufika mahakamani na hata simjui na sijawahi kumwona, afike mahakamani awe amelipa," alisema.

Shauri liliahirishwa hadi Januari 31 mwaka huu kwa ajili ya kusikilizwa maombi ya kumkamata mkurugenzi huyo ambayo yanatakiwa kuwa yamewasilishwa ndani ya siku saba kuanzia jana.

Awali mahakama ilitoa amri ya waandishi hao kulipwa baada ya kupitia hoja za washinda tuzo katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Julai 2023.

Shauri hilo namba 28461 la mwaka 2023, wadai ni Maregesi Paul na wenzake tisa dhidi ya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe.

Walalamikaji hao walipata tuzo Julai 17, 2023 mbele ya Msuluhishi wa CMA Ilala, Bonasia Mollel.

Madai ya awali yalikuwa jumla ya Sh. milioni 114. Baada ya kukaa mezani kwenye majadiliano kwa pamoja kiwango hicho cha fedha kilishuka na kufikia Sh. milioni 62.7.

Dudley alikubali kulipa fedha hizo kwa awamu tatu, Oktoba 30, Desemba 30 mwaka 2023 na awamu ya mwisho ilikuwa mwishoni mwa Februari mwaka jana, lakini hakulipa.

Dudley aliingia makubaliano ya kulipa malimbikizo hayo nje ya mahakama Aprili hadi Mei mwaka jana, lakini hajafanya hivyo.

KESI ZA UCHAGUZI

# Wataka Uchaguzi wa S/Mitaa urudiwe

**Na Kulwa Mzee**

WAGOMBEA watatu wa nafasi ya uenyekiti wa Serikali za Vijiji wilayani Mkuranga wamemburuta mahakamani Msimamizi wa Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakidai matokeo hayakuakisi mchakato halali wa uchaguzi, Katiba ilikiukwa na kulikuwa na kasoro nyingi za udanganyifu.

Wagombea hao kupitia Chama cha ACT Wazalendo wamefungua mashauri hayo na kuwasilisha madai yao mbele ya Mahakama ya Wilaya ya Mkuranga, wakiomba matokeo yafutwe na uchaguzi urudiwe ambapo juzi yalitajwa kwa Hakimu Mkazi, Kennedy Mrosso.

Katika mashauri hayo, wadai ni Mmbembu Saidi, Juma Kizigo na Bakari Mchonjo ambao waliwakilishwa mahakamani na Wakili Mwanaisha Zuberi.

Wajibu maombi katika shauri hilo ni Msimamizi wa Uchaguzi Kijiji cha Tambani, Kitongoji cha Mkoga na Kitongoji cha Mikengeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akiwawakilisha walalamikaji hao katika hati ya maombi, Wakili Mwanaisha Zuberi alidai Mmbembu aligombea na kushindwa Uchaguzi wa Serikali za Vijiji uliofanyika Novemba 27 mwaka jana katika kijiji cha Tambani.

Alidai kwa kuwa hakuridhika na mwenendo, vitendo na matokeo ya uchaguzi huo, aliwasilisha shauri hilo la uchaguzi akiomba kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi huo.

Alidai waleta maombi wote hawakuridhishwa na mwenendo na vitendo vya mjibu shauri namba moja ambaye ni msimamizi wa uchaguzi, ikiwamo kuwaengua nje ya wakati kinyume cha sheria na kanuni.

Mlalamikaji Bakari Mchonjo kabla ya kuondoshwa alikuwa mgombea uenyekiti katika kitongoji cha Mikengeni kupitia Chama cha ACT Wazalendo na Juma Kizigo alikuwa mgombea uenyekiti wa kitongoji cha Mkoga kupitia chama hicho.

Wakili alidai wajibu maombi ni maofisa kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji ambao majukumu yao ni kuhakikisha kanuni, mchakato na utaratibu wa uchaguzi vinafatwa na kuzingatiwa.

Alidai katika kijiji cha Tambani, mgombea wa CCM Nassib Said Makamba alitangazwa mshindi, matokeo ambayo hayakumridhisha Mmbembu anayedai kulikuwa na ukiukwaji mkubwa na ulio wazi wa kanuni za uchaguzi na misingi ya uchaguzi uliofanywa na mjibu maombi namba moja.

"Katika uchaguzi wa Novemba 27, 2024, mjibu shauri namba moja au watumishi wake walitoa matokeo yasiyoakisi mchakato halali wa uchaguzi ambao uliahidiwa na ambao ulipaswa kufuatwa, bali walitumia mchakato uliokuwa na upungufu mkubwa na ambao uliathiri matakwa halali ya wapigakura wa kijiji cha Tambani, kata ya Tambani, Halmashauri ya Mkuranga.

"Ukiukwaji wa kikatiba na kisheria uliofanywa na mjibu shauri wa kwanza, pamoja na kasoro nyingi na udanganyifu uliofanyika za kuwaengua nje ya muda waleta mashauri Novemba 22, 2024 ndani ya kampeni na kutokuwa wagombea kinyume cha sheria, kanuni na agizo la Waziri wa Tamisemi kwamba rufani zote mwisho ni Novemba 15, 2024.

"Kulikuwa na ukiukwaji wa kikatiba na kisheria uliofanywa na mjibu shauri wa kwanza, watumishi wake au mawakala wake, pamoja na kasoro nyingi na udanganyifu uliofanyika siku ya uchaguzi, ulisababisha mgombea aliyeshinda kutangazwa kinyume cha sheria," walidai walalamikaji.

Walalamikaji walidai msimamizi wa uchaguzi alikiuka Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Kamati ya Kijiji kwa kutotoa nakala za matokeo ya uchaguzi kwa mawakala kinyume cha sheria na kanuni za uchaguzi, kitendo ambacho kimewaathiri waleta maombi.

Walidai kulikuwa na kura bandia kwenye vituo ambapo wapigakura kadhaa walikamatwa nazo na taarifa ya kosa hili la kiuchaguzi iliripotiwa kwa askari, na miongoni mwa waliokamatwa na kura hizo zilizowekwa alama ya vyema kwa mgombea wa CCM ni Askari Kata Afande Lutebeka na ambaye pia alikuwa akiwatisha wapigakura.

Katika mashauri yao, wanadai wagombea wa CCM walitoa takrima za chakula na vinywaji kwa watumishi/maofisa ya uchaguzi vituoni, idadi halisi ya wapigakura kwenye vituo vyote tisa haikuwekwa wazi, kinyume cha sheria tajwa.

Ilidaiwa kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Kamati ya Kijiji, mjibu shauri namba moja anao wajibu wa kuhakikisha katiba, sheria, kanuni na miongozo inafuatwa katika kutekeleza majukumu yake na uamuzi wake ukijumuisha uamuzi wa kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Ilidaiwa mwenendo usiofaa ulioelezwa hapo juu, ikiwamo kuwaengua wagombea wa uenyekiti wa vitongoji vya Mkoga na Mikengeni nje ya muda uliofanywa na mjibu shauri namba moja ulifanywa kwa makusudi ya kumsaidia mgombea aliyemtangaza mshindi aweze kushinda Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji cha Tambani.

Waleta mashauri wanaomba mahakama kutoa amri kwamba uchaguzi ulikuwa batili kwa kukiuka kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Vitongoji na Wajumbe wa Kamati ya Kijiji na Vitongoji za Mwaka 2024.

Waliomba mahakama imwagize Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni mjibu shauri namba moja au yeyote anayehusika kuitisha uchaguzi mdogo wa Mwenyekiti wa Kijiji cha Tambani, Kitongoji cha Mikengeni Kata ya Tambani, Halmashauri ya Mkuranga ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya hukumu ya shauri hilo.

Pia waliomba mahakama itoe amri ya nafuu nyingine yoyote ambayo itaona ni ya haki na inafaa kutolewa.

Mashauri hayo yaliahirishwa hadi Januari 20 mwaka huu kwa ajili ya kuendelea na hatua zingine.

*Kwa maoni kuhusu habari hii na nyingine: +255 677 020 701 Email:customerrelations@guardian.co.tz*

**KABWELA** FADHILI MOHAMED



WASICHANA WAREJESHWA SHULENI...

# Waziri asema kuna idadi kubwa ya wavulana wanakatisha masomo

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAKATI serikali ikiwa imejikita kuwarejesha shuleni wanafunzi wa kike waliokatisha masomo kupitia Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP), imebainika kuwapo vijana wengi wa kiume wanaoendelea kukatisha masomo yao kutokana na sababu mbalimbali.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alisema hayo mjini Morogoro juzi wakati akizindua warsha ya tathmini ya utekelezaji kazi za mradi wa SEQUIP nchini.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, serikali imeweka mkakati wa kuwarejesha shuleni vijana hao wa kiume waliokatiza masomo kabla ya mradi huo kwisha na hata utakapomaliza muda wake.

Prof. Mkenda alisema kuwa kupitia SEQUIP, jumla ya wasichana 10,239 waliokuwa wamekatisha masomo wamenufaika kwa kurudi shuleni kuendelea na masomo.

"Wakati serikali inaendelea kutekeleza mpango wa elimu ya msingi ili kuishia darasa la sita ifikapo mwaka 2027, bado tunasisitiza umuhimu wa elimu ya msingi na sekondari, na sasa elimu hii itakuwa ni lazima kwa miaka 10," alisisitiza waziri huyo.

Alisema SEQUIP ni mradi wa kitaifa wenye malengo madhubuti ya kuinua viwango vya elimu na unalenga kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora inayokidhi mahitaji ya karne ya 21.

"Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari inayotolewa kwa njia mbadala, lakini malengo mahsusi ya mradi huu unaosimamiwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ni pamoja na kuongeza ufikiwaji wa wasichana walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari kutokana na sababu mbalimbali kama ugonjwa, mazingira magumu, kupata ujauzito au ndoa za utotoni kwa wenye umri kati ya miaka 13 na 21," alisema Prof. Mkenda.

Alisema mradi huo umelenga kuwafikia wasichana wapatao 12,000 nchini kote; kuwapatia wasichana na wavulana mazingira bora ya kujifunza na kuongeza ufaulu kwa wahitimu wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala.

Aliwaondoa hofu wazazi na walezi kuhusu vitabu vya kufundishia mitaala mipya na ya zamani kwamba vipo vya kutosha na uwiano ni kitabu kimoja kwa watoto watatu na tayari wadau mbalimbali likiwamo jeshi wameshirikishwa kusambaza vitabu hivyo ili vifike maeneo yote kwa wakati.

Mkuu wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) Prof. Michaeli Ng'umbi alitaja mafanikio mbalimbali kupitia mradi huo, yakijumuisha wasichana waliosoma elimu ya sekondari kwa njia ya mbadala wapatao 351 kujiunga na kidato cha tano na wasichana 218 kujiunga na vyuo vya kati.

Mapema Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa waraka namba mbili wa mwaka 2021 kuhusu urejeshwaji wanafunzi shuleni kwa waliokatiza masomo kwa elimu ya msingi na sekondari.

Alisema kuwapo SEQUIP kumesaidia sana serikali kufikia lengo la kuwarejesha wanafunzi shuleni hususani wasichana waliokatiza masomo.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (kushoto), akipokea zawadi ya ngao kutoka kwa Mkuu wa Chuo Taifa cha Ulinzi (NDC), Balozi Meja Jenerali Wilbert Ibuge, mjini Musoma juzi, alipofanya ziara ya mafunzo kwa vitendo mkoani humo, akiwa na viongozi, maofisa, wakufunzi na wanafunzi wa chuo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania imejaliwa rasilimali miradi jotoardhi

**Na Frank Monyo**

TANZANIA imeelezwa kuwa moja ya nchi zenye rasilimali kubwa kwa uwekezaji katika miradi ya jotoardhi, huku jumla ya megawati 30 zinatarajiwa kuingizwa kwenye gridi ya taifa mwaka wa fedha 2026/2027.

Hiyo inatokana na uwapo wa megawati 5,000 za nishati ya umeme na megawati 15,000 za matumizi ya moja kwa moja kwenye miradi ya jotoardhi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayeshughulikia umeme na nishati jadidifu, Dk. Khatibu Kazungu, wakati wa mkutano wa kimataifa wa masuala ya jotoardhi (Global Alliance), uliofanyika katika Baraza Kuu la 15 la Shirika la Kimataifa la Nishati Jadidifu (IRENA) Abu Dhabi, UAE.

Dk. Kazungu alisema kuwa Tanzania inalenga kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza katika uendelezaji wa nishati ya jotoardhi Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Akieleza zaidi kuhusu fursa zilizopo nchini Tanzania, Dk. Kazungu alisema kuwa rasilimali ya jotoardhi nchini inachangiwa na uwapo wa mikondo miwili ya Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, ambalo ni chanzo kikuu cha nishati hiyo katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tanzania imebaini maeneo 50 yenye viashiria vya uwapo wa rasilimali ya jotoardhi katika mikoa 16. Maeneo haya yako katika hatua mbalimbali za maendeleo kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi ya moja kwa moja," alisema Dk. Kazungu.

Dk. Kazungu aliwahimiza wabia wa maendeleo na taasisi binafsi kuwekeza Tanzania ili kuchangia upatikanaji wa nishati safi ya uhakika, endelevu, na rafiki wa mazingira.

Alibainisha kuwa serikali kupitia Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), ambayo ni kampuni tanzu ya TANESCO, imeipa kipaumbele miradi mitano ya kimkakati ili kuharakisha upatikanaji wa nishati ya jotoardhi.

Miradi hiyo ni pamoja ni: Ngozi (70 MW), Kiejo-Mbaka (60 MW, Mbeya), Songwe (38 MW, Songwe), Luhoi (5 MW, Pwani) na Natron (60 MW, Manyara).

Dk. Kazungu alifafanua kuwa miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na uhakiki wa rasilimali na utafiti wa kina.

Alisema kuwa uzalishaji wa umeme wa jotoardhi utaimarisha uchumi wa nchi, kulinda mazingira, na kuongeza kipato cha wananchi kupitia fursa za ajira.

Kwa sasa, Tanzania imejipanga kuimarisha miundombinu, ushirikishwaji wa sekta binafsi na wabia wa maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo unakamilika kwa ufanisi na kwa njia endelevu.

# RC Mara atangaza fursa kiuchumi mkoani kwake

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi amepokea viongozi, maofisa, wakufunzi na wanachuo wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) na kuwataka kuwa mabalozi wa kutangaza fursa mbalimbali za kiuchumi zilizomo mkoani humo.

Kanali Mtambi alisema hayo mjini Musoma juzi, wakati akipokea ugeni huo na kuuambia kuwa mkoa una fursa nyingi za kiuchumi katika sekta za utalii, madini, kilimo, viwanda na biashara.

"Ninyi wanafunzi wa kozi 13 kutoka NDC mpo katika ziara ya mafunzo kwa vitendo kwa muda wa siku sita. Ninawaomba mkawe mabalozi wa kutangaza fursa za kiuchumi mtakazoziona, kwani mkoa wetu pia una migodi ya madini katika wilaya zote," alisema Kanali Mtambi.

Aliwataka wageni hao kupata nyama choma na 'kichuri' ili kuonja ladha tamu ya nyama za mkoa huo na kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kujionea uzuri wa hifadhi hiyo inayopatikana mkoani humo.

Ninajua mtatembelea wilaya za Butiama, Tarime, Musoma na Serengeti lakini pia sekta mbalimbali ikiwamo kilimo, kumbukumbu na historia, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na nyumbani kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mtajionea mengi," alisema.

Aidha, aliwaomba wanachuo na wakufunzi kufanya upembuzi wa mambo ya kiutamaduni, kisiasa, kijamii na kiuchumi na kutoa mapendekezo watakapohitimisha ziara yao ya mafunzo mkoani humo.


"Niwaombe wananchi wa Mkoa wa Mara kutoa ushirikiano kwa kuwapokea na kuwapa msaada na taarifa zinazohitajika wakati wageni wetu wakiendelea na ziara yao," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Balozi Meja Jenerali Wilbert Ibuge, alisema chuo kinatoa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na muda mfupi kulingana na mahitaji ya taasisi husika.

"Katika mwaka wa masomo 2024/2025, chuo kina wanachuo 61 wa kundi la 13 ambao walianza mafunzo ya darasani Septemba, mwaka jana na wanatarajiwa kukamilisha mafunzo yao Julai, mwaka huu.

"Wanachuo 41 wanatoka Tanzania na wengine 15 wanatoka katika mataifa rafiki, lakini kwenye ziara hii wapo watano kutoka nje ya nchi, kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo," alisema Balozi Meja Jenerali Ibuge.

Balozi Meja Jenerali Ibuge alisema katika awamu hii, makundi ya yameshatembelea mikoa ya Mtwara, Kagera, Ruvuma, Katavi, Songwe, Pwani, Morogoro na sasa ni zamu ya mkoa wa Mara.



## M'kiti mpya awaangukia viongozi Mirerani

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

MWENYEKITI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani hapa Mkoa wa Manyara, Hans Nkya ameomba ushirikiano kwa wenyeviti na watendaji kufikisha huduma za afya kwa wananchi kwenye maeneo wanayoishi.

Pamoja na kuomba ushirikiano huo kwa wenyeviti hao wa vitongoji na watendaji wa mamlaka hiyo, Nkya, anakabiliwa na kibarua kingine cha kutatua changamoto ya wakazi hasa jamii ya Kimasai kukosa mwamko wa kupeleka watoto wao kujiunga na elimu ya msingi na ujenzi wa miundombinu ya madarasa katika vitongoji mbalimbali.

Akizungumza jana baada ya kuchaguliwa kushika wadhifa huo, aliwasihi wenyeviti na watendaji hao kumpa ushirikiano ili kuyapatia majibu matatizo ya jamii inayowazunguka.

Alisema jamii ya Mirerani ina changamoto kwenye sekta ya elimu, afya na huduma nyingine, hivyo wanapaswa kuhakikisha wanaondokana nazo.

"Sitakuwa na mtoto wa mgongoni wala wa mabegani wote mna haki sawa kwangu, hii nafasi nimepewa kama koti nikihisi joto nalivua na kukaa pembeni, hivyo tushirikiane kujenga Mirerani," alisema Nkya.

Mwenyekiti mstaafu wa Mamlaka hiyo, Adam Kobelo, alisema uchaguzi umepita na kuwataka wajumbe kuganga yajayo kwa mustakabali wa Mirerani.

"Nipende kumpongeza Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Simanjiro, Kiria Ormemei Laizer kwa kutumia maneno ya busara katika mchakato wa uchaguzi," alisema Kobelo

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Gracian Max Makota, alisema uchaguzi huo wa mwenyekiti na makamu wake umefanyika vyema.

"Changamoto zilizoongelewa hapa tutazichukua na zile ambazo tutaweza kuzitekeleza zitafanyiwa kazi kwa lengo la kuhakikisha maendeleo yanapatikana," alisema Makota.

Diwani wa Kata ya Endiamtu, Lucas Zacharia, alisema wajumbe hao wana kazi kubwa kuhakikisha sekta ya afya, elimu, maji na miundombinu inaboreshwa.

# Wafanyabiashara wa nyama wagoma

**Na Steven William,** MUHEZA

WAFANYABIASHARA wa nyama na wachinjaji wa ng'ombe na mbuzi wilayani hapa Mkoa wa Tanga wameingia katika mgomo baridi kupinga machinjio kukosa huduma ya majisafi ili kunusuru maisha yao na walaji.

Kutokana na ukosefu huo wa maji ya uhakika, wachinjaji na wafanyabiashara wanaopeleka mifugo yao kuchinjwa kwa ajili ya kuisambaza buchani, wameingia katika mgomo baridi kuishinikiza Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuboresha miundombinu ya maji katika machinjio hayo.

Akizungumzia jana malalamiko hayo, Katibu wa Jumuiya ya Wauza Nyama wa Wilaya hiyo, Omari Lutika, alisema wamelazimika kuchukua uamuzi huo kama njia ya kuushinikiza uongozi wa halmashauri hiyo kupeleka maji katika machinjio hayo yaliyopo Mtaa wa Sega.

Alisema juzi na jana,wafanyabiashara hao wameanzisha mgomo baridi kuchinja ng'ombe na mbuzi wakidai machinjio hayo hayana maji, licha ya kulipa ushuru wa serikali.

Akieleza undani wa mgomo huo, Lutika, alisema kitendo cha machinjio hayo kukosa maji ya uhakika, kunahatarisha afya yao, walaji na watu wengine wanaotoa huduma.

"Ni kweli tunapata tabu wachinjaji kusaka maji usiku mbali na machinjio kwa ajili ya kuosha utumbo na nyama nyingine. Hivi sasa watoa huduma katika machinjio ya Sega, wanalazimika kwenda kuchota maji Mto Mkurumuzi ambayo sio salama.

Tunaiomba Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuboresha huduma ya majisafi katika machinjio haya, pamoja na barabara inayoingia machinjioni, "alisema Katibu huyo.

Alipoulizwa kuhusiana na malalamiko hayo, Msimamizi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Nyama katika Machinjio ya Sega, Filbert Bwire, alithibitisha kuwapo kwa changamoto hiyo ya ukosefu wa maji.

"Hili jambo la kukosekana kwa maji ya uhakika katika Machinjio ya Sega, siyo la Halmahauri, ni la Mamlaka ya Maji inayotoa huduma hapa. Wao wamefunga mita ambayo haina uwezo wa kupandisha maji katika tangi.

Hata hivyo, walipewa taarifa kuhusu hii changamoto na wakaja kubadilisha mita ya kwanza na wameweka nyingine ya pili, lakini bado tatizo lipo pale pale, kwamba maji hayapandi kwenye tangi ili wayapate watumiaji."




Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Arusha, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Ally Jua, akisimamia zoezi la ukaguzi wa magari ya shule kwa lengo la kuepusha ajali, wilayani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majimbo kuchimbwa visima vya maji

**Na Allan Isack,** MANYARA

SERIKALI mkoani hapa inakusudia kuchimba visima vipya vitano vya maji kila jimbo ili kuboresha huduma hiyo kwa wananchi karibu na makazi yao.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Manyara, James Kionaumela alitangaza mpango huo wakati akizungumzia mikakati ya upatikanaji maji kwa jamii kwenye majimbo hayo.

"Serikali imeweka mikakati ya kila jimbo kwenye mkoa kuwa na visima vipya vitano kwa lengo la kuhakikisha maji yanapatikana karibu na wananchi," alisema Kionaumela.

Aliwataka wakazi wa majimbo hayo kutunza vyanzo vya maji ili viweze kuendelea kuhudumia kizazi cha sasa na kijacho.

Kionaumela, alisema jamii inapaswa kutunza vyanzo vya maji ili kuhakikisha miradi ya maji inaendelea vyema.

"Kulima karibu na vyanzo vya maji, kukata miti, kuchunga mifugo au kufanya shughuli nyingine kama hizo haitakiwi kwa jamii.

"Kwenye Mkoa wa Manyara, kutachimbwa visima 35 japokuwa hadi sasa vimeshachimbwa visima 29 na tunaendelea kuchimba vingine vilivyobaki," alisema Kionaumela.

Alisema RUWASA imejipanga kuhakikisha huduma ya maji inapatikana na kusambazwa kwenye vijiji vyote.


Aliwakumbusha wateja wao kulipa ankara ya maji waliyotumia kupitia mtandao wa RUWASA ili kuboresha utendaji kazi wake na huduma nyingine.

"Unapotumia maji na kutolipa ankara za matumizi yake, hautakuwa unafanya jambo sahihi, lipeni ili mamlaka iweze kujiendesha kwa maendeleo.

"Kuna mafundi ambao wanafanya ukarabati miundombinu ya maji ikiharibika, hivyo watu wanapopatiwa huduma na kulipa ankara pamoja na mengine, fedha hizo hutumika kuwawezesha," alisema Kionaumela.

Mkazi wa Kata ya Magara, Wilaya ya Babati, Idd Ntandu, alisema RUWASA ni miongoni mwa mamlaka zinazotoa huduma bora kwa jamii kwenye mkoa huo.

RUWASA Manyara inatoa huduma ya maji katika wilaya za Babati, Kiteto, Simanjiro, Mbulu na Hanang'.





# Tume ya Sefua yaanza kwa kilio cha utitiri wa kodi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

TUME ya Rais ya Maboresho ya Kodi imeanza kupokea maoni, kero, changamoto na mapendekezo ya wadau wa kodi nchini kwa kukumbana na kilio kikubwa cha utitiri wa kodi wanazotozwa na mamlaka za serikali mkoani hapa.

Wakitoa maoni yao juzi katika kikao cha kwanza kilichofanyika jijini hapa, wadau hao, wakiwamo wafanyabiashara, waliitaka serikali kupunguza utitiri wa kodi zenye mlengo mmoja na zinazosalia kuunganishwa na kuwa moja ili kuondoa usumbufu kwao.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa hoteli Mkoa wa Mwanza, Nyeriza Makongoro, alisema katika biashara hiyo kuna kodi zaidi ya 22 huku nyingine zikiwa na mwelekeo mmoja na kusababisha kuwapo kwa mianya ya rushwa.

"Nia yetu ni kulipa kodi ili kujenga nchi yetu, hali inayoendelea inasababisha wafanyabiashara kukwepa kodi na wakati mwingine kuilazimisha serikali kutumia nguvu katika ukusanyaji wa kodi," alisema Makongoro.

Mwenyekiti wa Chama cha Wavuvi Mkoa huo, Bakari Kadabi, alisema kundi hilo lina tozo zaidi ya 12, mtu mmoja analipa zaidi ya Sh. milioni 4.5 na kusababisha wavuvi kupungua kila kukicha.

Kadodi, aliomba kodi zote kuwekwa kwenye 'kapu' moja ili taasisi husika ziweze kukusanya fedha hizo katika eneo mmoja na mhusika akilipa asifuatwe tena.

Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa huo, Gabriel Kanene, alisema, utitiri wa kodi unakaribisha mazungumzo baina ya wafanyabiashara na maofisa wa serikali, hivyo kupunguza mapato ya taifa.

"Usumbufu wa kila taasisi kutaka kumfikia mfanyabiashara na namna gani wanamfikia hiyo ndiyo sababu ya tatizo kubwa tulilonalo kwa sasa," alisema Kanene.

Aliiomba tume hiyo kuishauri serikali kufumua sheria za faini na tozo kwa wafanyabiashara katika kiwango sawa bila kujali mitaji ya wahusika.

Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania Mkoa huo, Hamis Lugehe, aliomba Tume ya Kudumu ya kupokea malalamiko yao iundwe ili kuondoa dosari zinazojirudia mara kwa mara.

Lugehe, alisema tume hiyo ya sasa ina haja ya kuhakikisha kodi ya huduma ya asilimia 18 inapungua kwa kuwa ni kubwa ikilinganishwa na nchi nyingine asilimia 15 hadi 16 ili kuvutia wafanyabiashara.

Mshauri wa Walipakodi, Hadija Hassan, alisema ili kuleta unafuu kwa walipakodi na kuongeza mapato nchini, sheria za kodi zinatakiwa kupitiwa upya.

Hadija, alisema mifumo ya ulipaji kod nchini inatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuondoa faini kwa walipakodi kinyume cha sheria.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue, alisema lengo la kuundwa kwa tume yao ni kuhakikisha Taifa linaongeza ukusanyaji mapato kwa matakwa ya walipakodi.

Sefue, aliwakumbusha wafanyabiashara kujenga tabia ya kulipa kodi ili kuipa nguvu serikali kujitegemea kuboresha miundombinu hususan ya afya.

"Tanzania tija yetu ya kukusanya mapato bado ni ndogo ni kati ya asilimia 12 hadi 13 tu na haipaswi kuwa hivyo angalau tufikie asilimia 16 maana wananchi wanataka shule zijengwe, miundombinu ya afya iwepo tena ya kisasa, je tutafikaje huko kama hatutakua na fedha." alisema.



Mjumbe wa Bodi ya Taasisi ya Nyansaho Foundation ya wilayani Serengeti, mkoani Mara, Esher Mng'ori (wa pili kushoto), akikabidhi vifaa vya shule vya kuanzia kidato cha kwanza kwa mmoja wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu Esther Wambura, mjini Mugumu juzi. Watoto 55 walinufaika na msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 15. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali ya rufani yajengwa Nansio

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SERIKALI imeanza ujenzi wa hospitali ya rufani katika Kisiwa cha Nansio Wilaya ya Ukerewe kwa lengo la kuwaondolea adha wananchi kuvuka Ziwa Victoria kufuata matibabu ya kibingwa jijini Mwanza.

Akizungumza wakati wa kukagua utekelezaji wa mradi huo katika Kijiji cha Bukindo, Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Chagu Ng'oma alimtaka mkandarasi kukamilisha ujenzi kwa wakati na ubora.

Chagu, alimtaka mkandarasi huyo, M/S Dimetoclasa Real Hope Limited kuhakikisha mradi huo unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 25 unatekelezwa kulingana na thamani ya fedha hizo.

Alisema serikali imetenga fedha ili wananchi wa kisiwa hicho waweze kupata huduma za kibingwa jirani na maeneo yao badala kusafiri kwenda jijini Mwanza ambako ni mbali zaidi na kwa kutumia usafiri wa maji.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk. Jesca Lebba, alitoa wito kwa mkandarasi huyo na mshauri elekezi kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuwasilisha taarifa kila wapatapo changamoto ili kutatua kwa pamoja na kufikia lengo la serikali la kuwapatia wananchi huduma bora za afya na za kibingwa.

Wakala wa Usimamizi wa Ujenzi huo, Mhandisi John Bhoke aliahidi kujenga hospitali hiyo kwa kasi na kukabidhi kwa wakati kukidhi matakwa ya mkataba.

Mkandarasi huyo alikabidhiwa mradi huo Desemba 27, mwaka jana na kuahidi kukamilisha Juni 30, mwakani.

Serikali imetoa Sh.bilioni sita kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa mradi huo.

# Polisi yawataka abiria kudhibiti madereva wazembe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAMANDA wa Polisi mkoani mkoani hapa, Janeth Magomi, amewakumbusha abiria jukumu la kudhibiti madereva kukiuka sheria za usalama barabarani na ajali ili kunusuru maisha yao.

Kamanda Magomi, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni ya abiria paza sauti iliyofanyika katika kituo cha mabasi mkoani hapa kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani.

Alisema abiria wanatakiwa kutoa taarifa pale wanapoona dereva anakiuka sheria na kuendesha mwendo hatarishi badala ya kusubiri hadi itokee na kuanza kulalamika kuwa alikuwa haendeshi vizuri.

"Namba za kutoa taarifa zimebandikwa kwenye mabasi au trafiki akisimamisha basi toeni taarifa ili kuzuia ajali zitokanazo na uzembe wa dereva," alisisitiza Kamanda Magomi.

Kwa upande mwingine, aliwasihi madereva, kuhakikisha usalama wa abiria na kutambua maisha yao yapo mikononi mwao kwa kuwafikisha salama na kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Mwenyekiti wa Balozi wa Usalama Barabarani Mkoa wa Shinyanga, Seif Nassor, alisema ni jukumu la kila mmoja kutoa taarifa za ukiukaji wa sheria za usalama barabarani na madereva kuendesha kwa makini ili kupunguza ajali.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) Mkoa wa Shinyanga, Denis Magembe, aliwataka wamiliki wa mabasi na mawakala kutoa tiketi za mtandaoni kwa abiria ili kuepuka kutozwa nauli kubwa.

Baadhi ya abiria walidai mwendokasi husababishwa pia na baadhi ya askari wa kikosi cha usalama barabarani kutokana na baadhi ya wamiliki wa mabasi kununua njia na kwamba hata wakipaza sauti ni kazi bure.

Ukurasa 13



**MIKAKATI YAANZA KIELIMU KUPATA WATAALAMU KUFANIKISHA DIRA 2050**

Ukurasa 14



**TRUMP WHITE HOUSE**
**Kutinga tena Ikulu kibabe Jumatatu saa sita mchana**


# siasa

JUMATANO JANUARI 15, 2025

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


WADAU WASEMA

# Wakati CCM ikisaka mrithi wa Kinana, ni zama za kupata M/Kiti mwanamke

**Na Sabato Kasika**

KUANZIA Jumamosi wiki hii CCM, inakusudia kufanya Mkutano Mkuu Maalum ambao matokeo yake ni pamoja na kujaza nafasi ya Makamu Mwenyekiti Bara.

Nafasi hiyo iliachwa wazi na Abdulrahman Kinana mwaka jana, aliyetangaza kujiuzulu na sasa chama kinaziba pengo hilo.

Wakati maandilizi yakiendelea, kuna baadhi ya majina yanayotajwa kwamba huenda miongoni mwao wakamrithi mwanasiasa huyo.

Licha ya majina yanayotajwa huku na kule, wapo baadhi ya wadau wa siasa wanaosema kuwa ni nyakati za usawa wa kijinsia na sasa nafasi hiyo ishikiliwe na mwanamama ili naye aonyeshe uwezo wake wa kukiongoza chama.

Baadhi ya wadau wa siasa na watetezi wa haki za wanawake na uongozi wanaotoa mchango wao ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga.

Anasema tangu uhuru, chama hicho hakijawahi kuwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa mwanamke, na kwamba ni vyema sasa akapatikana.

Dk. Anna anasema hata kama mwenyekiti na makamu wake wakiwa wanawake si vibaya, kwa maelezo kwamba miaka yote katika nafasi hiyo wamekuwa ni wanaume na sasa ni vyema kinamama kushika nafasi hiyo.

Anasema suala la uongozi wa 50/50 lianze na lionekane kwenye ngazi za juu ili umma uione dhamira ya Tanzania kuwa na usawa wa kijinsia kwenye uongozi.

Hata hivyo, mkurugenzi mtendaji huyo anatoa angalizo kuwa asiwe ilimradi mwanamke bali awe ambaye ana uwezo wa kuongoza, na kwamba hilo ndilo jambo la msingi linalopaswa kuzingatiwa.

"Sio kila mwanamke anafaa kuwa kiongozi bali kinachotakiwa kuzingatiwa uwezo wake wa kuongoza na ninaamini kuwa ndani ya chama hicho wapo wanawake wa aina hiyo," anasema Dk. Anna.

Anatamani kuona angalau nafasi hiyo inakuwa chini ya mwanamke ili kuendeleza kile ambacho chama kilianzisha tangu kuwa na makamu wa rais mwanamke na sasa ni Rais Mama Samia Suluhu Hassan.

Hatua hiyo ndiyo imefikia kuwa na mwenyekiti wa chama taifa mwanamke sasa, na kwamba mwendelezo huo ungefikia kuwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara mwanamama.




Moja kati ya mikutano maalumu ya CCM jijini Dodoma. **PICHA :MTANDAO**

**SAA YA WANAWAKE**

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, Seleman Bishagazi, anasema sasa ni wakati sahihi kwa chama hicho kumpata makamu mwenyekiti mwanamke.

Anaongoza kuwa wanawake wengi wameelimika kuhusu masuala ya uongozi wa kisiasa, kiuchumi, kiteknolojia na hilo linawezekana.

"Vuguvugu la harakati za kutafuta usawa wa kijinsia katika uongozi, limesaidia kuwafanya wanawake kuwa na uelewa wa kutosha wa masuala ya uongozi, hivyo kwa mtazamo wangu ninaona ni zamu ya wanawake kuongoza CCM kwa sababu wapo," anasema Bishagazi.

Mbali na hilo, anasema wapo wasomi wanawake wengi katika chama hicho ambao wanaweza kukabidhiwa majukumu wakayatekeleza kwa ufanisi kama ambavyo wanaume wanafanya au pengine hata kuwazidi.

"Uongozi si mzigo wa kubeba begani au kichwani bali uwezo wa kuongoza, elimu na busara ninazoamini kuwa wanawake wengi wanazo lakini bado wameachwa nyuma hasa katika vyama vya siasa," anasema.

Bishangazi anafafanua kuwa kwa kuwa tangu kuanzishwa kwa TANU hadi CCM hajawahi kuwapo makamu mwenyekiti wa chama mwanamke, Mkutano Mkuu Maalum wa chama hicho kwa mara ya kwanza uweke mwanamke asaidiane na Rais Samia, kukiongoza chama.

"Mimi ni mwanaharakati ninazunguka maeneo mbalimbali ninaona jinsi wanawake walivyo na mwamko katika uongozi. Nina imani nao kuwa wanaweza kuongoza," anasema.

**SI LAZIMA**

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Dk. Ananilea Nkya, anasema uongozi hauna jinsi bali kinachotakiwa ni kuwa na uwezo na sifa.

"Kwenye suala la uongozi, siangalii mwanamke au mwanaume kwa maumbile yake bali ninaangalia kama ana sifa ya uongozi. Hivyo, hata CCM wanapaswa kuzingatia hilo," anasema Ananilea.

Anasema kusukumwa na mtazamo wa mwanamke au mwanaume bila kuzichunguza sifa za mtu katika uongozi, kunaweza kusababisha ombwe na hata kuliangamiza taifa kwa kuongozwa na watu wasio na sifa na wala vigezo.

Kama nilivyoanza kueleza, kwangu mwanamke au mwanaume kwa maumbile, si kigezo cha kuwa kiongozi, bali uwezo na sifa za kuongoza ndivyo vinavyopswa kuzingatiwa," anasema.

Mwenyekiti huyo anataja baadhi ya sifa za kiongozi kwamba ni kuwa na karama na uwezo wa kuongoza, mkweli, anayejitambua, msimamizi wa maamuzi, msikilizaji na awe na umoja na wale anaowaongoza.

"Kwa ujumla sifa zipo nyingi kwa wanawake na wanaume, lakini tusing'ang'anie mwanamke au mwanaume kwa maumbile bali sifa za kuongoza ndizo ziwekwe mbele ili kupata kiongozi bora," anasema.

Anasema pamoja na sifa hizo, kiongozi anatakiwa kuwa na elimu itakayomwezesha kufanya kazi kwa ufanisi, na kwamba hata ndani ya CCM wapo watu wa aina hiyo, huku akifafanua kuwa upatikanaji wa makamu mwenyekiti CCM taifa usisukumwe na jinsia.

"Awe mwanamke au mwanaume wote wanafaa kuongoza ili mradi sifa za uongozi zizingatiwe bila kuegemea katika masuala ya jinsia ambayo yanaweza kusababisha asipatikane kiongozi bora ikiwa bora kiongozi anasema.

# MUHTASARI WA RASIMU YA DIRA YA TAIFA 2050



Treni ya mwendokasi ni miongoni mwa mikakati ya dira ya kuwa na Tanzania yenye miundombinu bora. **PICHA: WUC**

**NA MWANDISHI WETU**

KATIKA kipindi cha miaka 25 iliyopita, Tanzania imetekeleza dira ya maendeleo ya taifa 2025, ambayo ililenga kuinua uchumi wa nchi hadi hadhi ya kipato cha kati.

Dira hiyo iliyoanza kutumika mwaka 2020 inafikia ukomo na sasa taifa limeanza nyingine ya 2050.

Kupitia dira hiyo, Tanzania ilifanya mengi ikidhamiria kufanya mageuzi makubwa ya kimaendeleo ya kijamii na kiuchumi ambayo yatalingana au kuzidi ya nchi za kipato cha kati ngazi ya juu.

Ili kufikia lengo hilo, rasimu ya dira 2050 inasema Tanzania imedhamiria kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati ngazi ya juu, ikichagizwa na sekta ya uzalishaji viwandani.

Lengo ni kufikia pato la mtu la kati ya Dola za Marekani 4,700 sawa na Sh. milioni 11.6 hadi 8,000 karibu Sh. milioni 19.8, huku pato la taifa likifikia zaidi ya dola za Marekani bilioni 700, ifikapo 2050.

Kuondoa umaskini uliokithiri na kupunguza kiwango cha umaskini wa mahitaji kuwa wa chini ya asilimia tano. Tanzania kuwa nchi kinara katika uzalishaji wa chakula barani Afrika na kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa 10 wa chakula duniani.

Vilevile, shabaha nyingine ni kuwa na mazingira bora ya kufanya biashara na kushika nafasi ya tatu kwa ubora barani Afrika katika kuvutia wawekezaji.

Aidha kuwa na sekta binafsi imara na yenye ujasiri na uwezo wa kiushindani,
kikanda na kimataifa. Pamoja na hayo shabaha nyingine ya dira ni kukifanya Kiswahili kuwa lugha inayoheshimika na kutumika ukanda wa Afrika Mashariki na moja ya lugha rasmi zinazotumika kwenye Jumuiya ya Umoja wa Mataifa.

Kuwa na mfumo bora wa elimu katika ngazi zote unaojenga maarifa na stadi za wahitimu na wenye kushabihiana kwa karibu na sekta za uzalishaji. Aidha, kuwa na jamii yenye afya njema ambapo kila Mtanzania anapata huduma bora za afya, maji na hifadhi ya jamii.

Kuwa taifa linalojitehemea kwenye umeme ambapo wastani wa matumizi ya uememe wa mtu ninafsi yatakuwa angalau kilo wati 600 kwa saa.

Pia shabaha nyingine ya dira 2050 ni kuwa na jamii inayothamini kuhifadhi mazingira na iliyotayari kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Tanzania kuwa kitovu cha huduma za usafirishaji shehena katika ukanda wa Afrika, kuwa na jamii yenye maarifa ya kidijitali na uwezo wa kutumia zana na kuzalisha teknolojia ya kidijitali katika huduma za uzalishaji.

Shabaha nyingine ya dira hii ni kuifanya Tanzania kuwa taifa la kidemokrasia likiongozwa na katiba imara inayoakisi mwafaka wa kitaifa, taasisi madhubuti za umma na mfumo thabiti wa vyama vingi vya siasa, shabaha nyingine ni Tanzania kuwa miongoni mwa mataifa 10 bora duniani na kushika nafasi ya kwanza barani Afrika katika kupunguza pengo la kijinsia kwa asilimia 35 ifikapo mwaka 2050.

Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kwa wanaume na wanawake kufikia miaka 75, kadhalika kuwa kinara barani Afrika kwenye vivutia watalii na miongoni mwa nchi bora Afrika zinazotembelewa na watalii kwa wingi.

> Maeneo ya kuzingatia ni pamoja na kuwapo sera za fedha, mapato na kodi zenye kutabirika zitakazozingatia uwiano, vigezo muhimu kama mapato na matumizi, urari, akina na uwekezaji, uzalishaji na mahitaji.

Kila Mtanzania kuwa na elimu angalau kidato cha nne na angalau asilimia 15 ya Watanzania kuwa na elimu ya juu wakiwa naujuzi stahiki unaolingana na mahitaji ya soko la ajira na dunia inayobadilika, angalau mmoja katika Watanzania wawili mwenye sifa za kuajiriwa katika sekta rasmi na wakiwa na mikataba kamili ya ajira.

Shabaha nyingine ya dira 2050 ni Watanzania wote wafurahie uhuru wa kutoa maoni na uhuru wa kukusanyika katika mazingia ya amani usalama na utulivu.

Wakati shabaha ya mwisho ni ardhi yote ya Tanzania kupangwa na kupimwa kwa matumizi mbalimbali. Kwa ajili ya makazi bora kilimo, mifugo na uwekezaji

**MUUNDO/MALENGO**

Dira ya 2050 imegawanyika katika maeneo manne ya msingi mkuu ambayo ni utawala, amani, usalama na utulivu.

Eneo hili ndilo jiwe na msingi linalobeba mengine yote kwa hiyo kuyumba eneo hilo kutayumbusha mengine yote.

Nguzo kuu zinazobeba dira ziko tatu nazo ni uchumi imara, jumuishi na shindani, pia kuwa na watu wenye uwezo, maendeleo ya jamii, uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu kwenye mabadiliko ya tabianchi.

Kufikiwa kwa malengo ya dira 2050 kunategemea ufanisi wa utekelezaji wa nguzo hizo.

**VICHOCHEO**

Haya ni maeneo yanayochochea kasi ya utekelezaji wa maeneo mengine ya dira ili kuleta tija, ufanisi na ubunifu.

Navyo ni pamoja na sekta za kimageuzi ambazo pia huitwa sekta kipaumbele ambazo utekelezaji wake unategemewa kuchagiza na kuwezesha ukuaji wa uchumi kufikia lengo la taifa la kuwa na uchumi wa kati wa ngazi ya juu.

Aidha, lengo la msingi mkuu wa dira hii ni kuwa na mifumo imara ya kisheria na kitaasisi katika kuwezesha utekelezaji endelevu na wenye ufanisi wa dira 2050.

Maeneo yatakayozingatiwa ni utawala bora na haki za jamii. Katika ngazi mbalimbali serikalini na taasisi za mifumo yote ya kijamii itakayohamasishwa na kuwepo na utawala wa sheria, demokrasia, kupinga unyanyasaji wa aina zote, kupiga vita rushwa na kudumisha uhuru wa Asasi za Kiraia (AZAKI).

Aidha, kuwa na serikali imara za mitaa zenye ufanisi ni sehemu ya dira hiyo, zinazojitegemea, zenye ubunifu, kuzingatia maadili ya utumishi wa umma na zinazowajibika na kutoa huduma bora kwa jamii.

Uwajibikaji katika utumishi wa umma, sifa hii inayoongozwa na matamanio ya kuwapo watumishi wa umma wenye maadili, kuzingatia weledi na utawala wa sheria.

Vile vile dira inasisitiza umuhimu wa raia kuzingatia sheria na kupiga vita maovu.

Aidha, amani usalama na utulivu ili kuwepo kwa taifa imara, tulivu lenye umoja licha ya tofauti za dini, kabila na jinsia ni sehemu ya dira hiyo.

Kadhalika kufikia taifa lenye watu wenye uwezo wa kubaini fursa, kutabiri matukio mapema ili kuweka mifumo madhubuti na kujikinga na majanga na kulinda maslahi ya taifa.

Nguzo ya kwanza ya uchumi imara, jumuishi na shindani lengo lake ni kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuimarisha ushindani na uwazi na kuwezesha utabiri wa sera za kiuchumi kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kufikia uchumi imara, jumuishi na endelevu.

Maeneo ya kuzingatia ni pamoja na kuwapo sera za fedha, mapato na kodi zenye kutabirika zitakazozingatia uwiano, vigezo muhimu kama mapato na matumizi, urari, akina na uwekezaji, uzalishaji na mahitaji.

Ubunifu katika vyanzo mseto vya mapato. Katika eneo hili matamanio ni kuimarisha ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi pamoja na soko la fedha katika kugharamia shughuli za maendeleo.

Kuwapo na mazingira yenye kuvutia, kulinda, kuendeleza uwekezaji na biashara, yatakayowezesha kuwapo kwa sera endelevu na zinazotabirika pamoja na kupunguza gharama za uwekezaji na biashara.

Aidha, kuanzisha mashirika ya umma ya kimkakati na kuwa na mashirika ya umma madhubuti na yenye ufanisi , viongozi na watendaji waadilifu, kuendeshwa kwa uwazi na uwajibikaji ni shabaha ya dira.

Kadhalika mashirika hayo yafanyekazi kwa uwazi, kuvutia uwekezaji mbalimbali na kuzingatia faida ili kuharakisha maendeleo kiuchumi na utoaji wa huduma za umma ndicho dira inachotazamia.

*ITAENDELEA WIKI IJAYO*

# Mikakati yaanza kielimu kupata wataalamu kufanikisha dira 2050

**NA GRACE MWAKALINGA**

BAADA ya kuiaga 2024 na kuikaribisha 2025, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kuliendeleza taifa kuanzia kwenye sekta ya elimu ndiyo suala la kipaumbele.

Kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo dunia imeshuhudia, bila shaka Tanzania inatarajia mambo makubwa zaidi katika tasnia ya teknolojia yanayohitaji kusimamia TEHAMA kwenye kufundisha ili kufanikisha kutekeleza dira ya maendeleo ya taifa ya 2050.

Ndiyo maana katika juhudi za kuboresha masomo ya sayansi na teknolojia, serikali inawapa mafunzo maalum walimu wa sayansi, TEHAMA, kupitia mradi wa kuimarisha elimu ya sekondari (SEQUIP).

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Mahera, anatinga Tarime mkoani Mara, kufungua mafunzo ya walimu wa masomo hayo wa mikoa ya Mara na Simiyu.

Lengo la mafunzo ni kuwawezesha walimu kutumia mbinu za kisasa za ufundishaji, kama TEHAMA kuongeza ufanisi na ujuzi wa wanafunzi katika masomo ya sayansi, hisabati na teknolojia, ili kuwaandaa kuwa wataalamu na wavumbuzi wa masuala mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Dk. Mahera anasema hizo ni jitihada za kuhakikisha walimu wanapata mafunzo ya kisasa yanayoboresha mbinu za ufundishaji.

Anasisitiza kuwa mafunzo hayo ni muhimu ili kuboresha ufundishaji sayansi, hisabati na TEHAMA, ili kuwajengea uwezo wa kuandaa na kutumia zana bora za kujifundishia na kujifunzia kutokana na mazingira yao.

Dk.Mahera anafafanua kuwa, hadi sasa walimu zaidi ya 29,000 wameshanufaika na mafunzo hayo, na lengo ni kuwafikia walimu 40,000 ifikapo Januari 2026.

"Mafunzo haya, yanahusisha matumizi ya teknolojia ya kisasa kufundisha, ambayo yatawezesha walimu kuwafundisha wanafunzi kwa njia bora zaidi na kuwaandaa kuwa wataalamu wa sayansi, hisabati na TEHAMA katika siku zijazo," anasema Dk. Mahera.

Anawasisitiza walimu, kumudu matumizi ya Kiingereza katika kufundisha na kujifunza TEHAMA.

Mratibu wa Mradi wa SEQUIP, Dk. Nicholaus Gati, anasema mradi huo unakusudia kuboresha mazingira ya elimu kwa wanafunzi wa sekondari na kuhimiza matumizi ya teknolojia za kisasa kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Anasema malengo ya mradi ni wanafunzi, hususan wa kike, wapate elimu ya sekondari na kumaliza masomo kwa mafanikio.

"Mradi huu ni wa miaka mitano, ulianza Novemba 2021 na utakamilika Januari 2026 kwa kutumia Sh. trilioni 1.2, tutaongeza fursa za elimu kwa wasichana ili wapate elimu ya sekondari kwa usawa na kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwenye elimu ya sekondari," anasema Dk. Gati.



Mwezeshaji wa soma la TEHAMA Julieth Kiwelu, akifundisha walimu kwa vitendo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

Mkurugenzi wa Ualimu, Huruma Mageni, anasema walimu wamefundishwa kutumia mbinu za kisasa ambazo zinakuza ubunifu, kutumia TEHAMA, ili kuwawezesha wanafunzi kufikia malengo kwa ufanisi na urahisi zaidi.

"Kwa kuzingatia juhudi zinazofanywa katika kuboresha elimu ya sekondari kupitia mbinu shirikishi na mafunzo endelevu kwa walimu, kuna matumaini makubwa ya kuongeza ufanisi katika masomo ya sayansi, hisabati na teknolojia," anasema Mageni.

Ni muhimu katika kukuza uwezo wa wanafunzi, ili kuwaandaa kuwa wataalamu na wabunifu wenye ujuzi wa masuala mbalimbali, mafunzo hayo, yanaweka msingi wa maendeleo ya kitaaluma na kiuchumi, ambayo yatajenga jamii yenye ufanisi na uwezo wa kukabiliana na changamoto za kisasa duniani.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, mhadhiri mwandamizi wa fizikia kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu (MUCE) cha mkoani Iringa, Dk. Talam Kibona, anasema ni hatua muhimu ya kuleta mabadiliko katika ufundishaji wa sayansi na teknolojia.

Anasisitiza kuwa bila fizikia, si rahisi kupata wataalamu kama wahandisi, madaktari au marubani, na kwamba walimu waliojengewa uwezo wa kufundisha masomo hayo kwa ufanisi watakuwa na mchango mkubwa katika kuwatengeneza wataalamu wa fani hizo kwa mustakabali wa taifa.

Dk. Kibona anaongeza kuwa mabadiliko ya mitaala yanalenga kuendana na mahitaji ya kisasa ya elimu, ambapo Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza katika kutoa elimu bora kwa nchi zinazoendelea.

Mhadhiri mwandamizi, Idara ya Kemia, UDSM, Dk. Grace Kinunda, anaeleza kuwa mafunzo waliyoyatoa yanawawezesha walimu kutumia mbinu mbalimbali shirikishi kwenye ufundishaji na ujifunzaji, kwa vitendo.

Anasisitiza kuwa, kupitia mbinu hizo kemia itakuwa rahisi kueleweka na kupendwa na wanafunzi ukilinganisha na ilivyokuwa awali kabla ya walimu kujengewa uwezo wa kutumia mbinu za kisasa kwa vitendo katika ufundishaji.

"Kwa muda tuliokaa darasani na walimu wameona kuwa mbinu hizi zitamaliza mada kwa ufanisi, hata katika madarasa makubwa, na kuwafanya wanafunzi kushirikiana na kutafakari pamoja kwa kina," anasema Dk. Grace.

Aidha, katika mafunzo hayo Grace anawasisitizia walimu, umuhimu wa kutumia vifaa vilivyopo katika mazingira yao, badala ya kutegemea vifnavyotoka viwandani wanapofanya majaribio ya kemikali.

Anasema juhudi zitapunguza gharama na kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali zilizopo.

Anaonyesha wasiwasi kuhusu ushiriki mdogo wa walimu wanawake katika mafunzo hayo na kusema ni muhimu kuongeza idadi yao ili kuondoa dhana potofu katika jamii kuwa masomo ya sayansi ni ya wanaume pekee.

Anakazia umuhimu wa kuwajumuisha walimu wenye ulemavu katika mafunzo hayo akisema ni muhimu kushiriki kwa wingi ili wajifunze kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na kuwasaidia wanafunzi wao, bila kujali changamoto yoyote waliyonayo.

Dk. Lilian Mulamula, Mhadhiri wa Idara ya Bailojia UDSM, anaeleza kuwa matumizi ya TEHAMA ni kiungo kufanikisha ufundishaji wa kisasa, kwani inawasaidia walimu kuandaa zana mbalimbali za kufundisha kwa vitendo.

Anasema teknolojia hiyo, inawawezesha wanafunzi kushiriki kikamilifu katika darasa, jambo ambalo linajenga ufanisi na kuelewa somo kwa vitendo.

"Moja ya mabadiliko makubwa yaliyoletwa na mafunzo haya ni matumizi ya teknolojia katika kufundisha na kujifunza, walimu wamejengewa uwezo wa kutumia vifaa vya kisasa kama kompyuta, simu na picha mjongeo katika ufundishaji wao," anasema Dk. Lilian.

Dk. Jason Mkenyeleye ni mhadhiri mwandamizi Idara ya Hisabati na Takwimu Chuo Kikuu cha Dodoma, anayeeleza kuwa mafunzo hayo yameboresha mbinu za ufundishaji za walimu ikilinganishwa na hali ilivyokuwa awali.

Anasema walimu sasa wana uwezo wa kuandaa na kutekeleza shughuli zao kwa kutumia zana za kisasa, kulingana na mabadiliko ya mitaala, pamoja na kuzingatia matumizi ya TEHAMA.

### CHANGAMOTO

Anazieleza kuwa ni walimu walioshiriki mafunzo baadhi yao kukosa vifaa vya TEHAMA, jambo linalozuia utekelezaji wa mbinu mpya.

Dk. Mkenyeleye anasisitiza kuwa ni muhimu kwa shule kupata vifaa hivyo kwa wingi, ili walimu wavitumie na mbinu bora za kufundisha.

Mwalimu wa hisabati kutoka Shule ya Sekondari Binza, mkoani Simiyu, Mzee Luchagula, anasema wamejifunza mbinu za kisasa za ufundishaji, zikiwamo matumizi ya teknolojia, ambazo zitawawezesha kushirikisha wanafunzi zaidi darasani.

Anaongeza kuwa, kwa kutumia mbinu hizo, wamepata uwezo wa kumudu darasa lenye wanafunzi wengi kwa kutumia teknolojia na kukabili ulemavu alionao.

Thimon Baitu, anayefundisha fizikia katika Shule ya Sekondari Meatu, mkoani Simiyu, anasema mafunzo hayo yamewasaidia kutambua umuhimu wa kutumia TEHAMA mfano video za msisimko wanapofundisha.

Anasema kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataelewa kwa urahisi mada za fizikia, ingawa anaitaja changamoto ya kukosa vifaa vya TEHAMA na intaneti kuwa kikwazo.

Mwalimu wa Hisabati Sekondari ya Busangwa, Fathiya Shah, anaeleza kufurahia mabadiliko ya mitaala ambayo yamewezesha walimu kujifunza TEHAMA kufundisha.

"TEHAMA, itawasaidia wanafunzi kuelewa vizuri hisabati kwa njia ya vitendo, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa wakitegemea nadharia pekee," anasema.

Kutoka Sekondari ya Nkololo, mkoani SImiyu, mwalimu Nyandamboje Lulyalya, anayeishi na ulemavu anasema mafunzo hayo yamempa ujuzi wa kutumia vifaa vinavyopatikana katika mazingira yake kufundisha kwenye maabara.

Anasema mbinu za kufundisha kwa kushirikisha wanafunzi zitaongeza ufanisi katika kujifunza kemia.


Aidha, anataja ukosefu wa vifaa na ujuzi wa walimu kufundisha somo hilo kwa vitendo kuwa ni changamoto, akiomba mafunzo hayo kuendelea ngazi ya wilaya ili walimu wengine wanufaike.

Mdhibiti Ubora kutoka Wilaya ya Rorya, Masanja Mashimba, anaongeza kuwa mafunzo hayo yatasaidia walimu kutumia mbinu za kisasa na kusimamia ufundishaji bora.

TRUMP WHITE HOUSE

# Kutinga tena Ikulu kibabe Jumatatu saa sita mchana

**Na Christina Mwakangale**



Donald Trump akila kiapo Ikulu ya Marekani Washington, D.C. Januari 20, 2017. **PICHA: WHITE HOUSE**

WIKI ijayo inaweza kuitwa ni ya Donald Trump. Kwani kile alichokitaka amekipata. Ni urais wa Marekani anaoupambania kwa nguvu zote, licha ya wabaya wake kutishia kumuua kwa risasi akiwa jimboni Pennsylvania, wakati wa kampeni.

Anakula kiapo Jumatatu ijayo. Anatinga ikulu akiwa Rais wa Marekani wa 47. Anaingia na historia ya kuwa rais wa pili kurudi madarakani katika vipindi visivyofuatana.

Jarida la Times Magazine la Marekani linabainisha hayo, kwamba Trump na Grover Cleveland, ndiyo marais pekee nchini humo, kuingia madarakani kwa vipindi tofauti visivyofuatana.

Cleveland aliongoza Marekani kuanzia 1885-1889 na kurejea tena madarakani 1893 hadi 1897. Kwa mujibu wa jarida la Times Magazine.

TRUMP

Donald Trump (78), Januari 20, anaapishwa kuwa rais rasmi, akipokea kijiti kutoka kwa Rais Joe Biden.

Trump alishika mamlaka hayo lakini mwaka 2020 aliwekwa pembeni akiwa rais wa 45 wa nchi hiyo yenye nguvu kiuchumi duniani.

Zikisalia siku chache, Trump kuingia Ikulu ya White House, inakadiriwa watu kadhaa watahudhuria na mamilioni kushuhudua kupitia vyombo vya habari kwenye mitandao na runinga duniani kote.

Inakadiriwa kwamba watu milioni 31 walijumuika kushuhudia sherehe za kuapishwa kwa Donald Trump Washington D.C., Ijumaa, Januari 20, 2017.

Uapisho wa Barack Obama, muhula wa pili uliofanyika Januari 21, 2013, ulivutia watazamaji milioni 20.55 huko Marekani. Na uapisho wake wa kwanza Obama, watu milioni 38 walishuhudia na kuwa wa pili kufuatiliwa zaidi baada ya ule wa Ronald Reagan, mwaka 1981.

Ingawa kuna maswali ya wadadisi kwamba je, Trump, atavunja rekodi ya Barack Obama, kuwa na wafuatiliaji wengi duniani wakati akiapishwa.

Trump, ambaye alimdhibiti Makamu wa Rais, Kamala Harris katika uchaguzi mkuu wa 2024, alithibitishwa kama mshindi wa uchaguzi huo wakati wa kikao cha pamoja cha Congress, Januari 6, mwaka huu, wiki ijayo anarudi katika Ikulu ya White House.

Kulingana na masharti ya mabadiliko ya 20 ya Katiba ya Marekani, rais mpya anachukua rasmi madaraka saa sita mchana, Januari 20, 2025. Awali rais mpya alikuwa anachukua madaraka Machi 4.

**KINACHOJIRI UAPISHO**

Rais anayeondoka madarakani, kwa kawaida hutembea pamoja na rais mteule hadi jengo la bunge, kwa ajili ya sherehe ya kuapishwa.

Rais anayeondoka ataacha ujumbe kwenye Ofisi ya Rais anakofanyia kazi na shughuli zake iitwayo Oval Office ili mrithi wake anayeingia kazini ausome.

Kawaida, makamu wa rais hula kiapo chake kwanza, kisha rais mteule anafuata.

Kiapo hicho kinafanyika karibu na saa sita mchana, siku ya kuapishwa, ili kuendana na wakati rasmi rais mpya anapochukua madaraka.

Baada ya viapo vya madaraka, rais mpya hutoa hotuba ya kuapishwa, anaandika masuala yake vya kwanza vya kisheria katika sherehe ndani ya bunge, na kisha anashiriki kwenye maandamano yanayojaa mitaani ya Washington. Umma hukaribishwa kushiriki kwenye tukio hilo kubwa.

**MAANDALIZI**

Tangu mwaka 1901, Kamati ya Pamoja ya Congress kuhusu sherehe za kuapishwa, imeshughulikia maelezo mengi ya sherehe za rais kuapishwa madarakani.

Kamati hiyo ina wanachama kutoka vyama vya kisiasa vyote vya Marekani. Kundi la mwaka huu linajumuisha Spika wa Baraza la Wawakilishi Mike Johnson, Kiongozi wa Wengi wa Seneti Chuck Schumer.

**USHINDI WA TRUMP**

Kinyang'anyiro kati yake na mgombea wa Chama cha Democratic Kamala Harris, kilidhaniwa kuwa cha ushindani mkali lakini matokeo ya uchaguzi yalionesha kuwa Trump amepata kura za kutosha kushinda.

Atakuwa rais wa kwanza wa zamani kurejea madarakani kwa zaidi ya miaka 130, akiwa na miaka 78, kuchaguliwa katika wadhifa huo.

Viongozi wa dunia walipongeza Trump kwa ushindi wa uchaguzi wa rais Marekani miongoni mwao Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu na mwenzake wa Uingereza, Keir Starmer.

Kulikuwa na hofu kwamba ushindani mkali kati ya wagombea katika baadhi ya majimbo muhimu ungeibua maswali mengi kuhusu matokeo ya uchaguzi huo.

Lakini mambo yaligeuka ghafla katika majimbo ya North Carolina, Georgia, Pennsylvania na Wisconsin, pamoja na ushindi katika majimbo ambayo yamekuwa yakiunga chama cha Republican, ulimwezesha Trump kufikia idadi ya kura 270 ya wawakilishi maalum wanaohitajika kushinda uchaguzi wa urais.

Trump sasa ni rais mteule, na mgombea mwenza wake James David Vance au JD Vance anakuwa makamu wa rais mteule, ambao watakuwa viongozi rasmi Jumatatu ijayo. Baada ya kuapishwa, rais mpya anaanza kazi mara moja.

> Viongozi wa dunia walipongeza Trump kwa ushindi wa uchaguzi wa rais Marekani miongoni mwao Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu na mwenzake wa Uingereza, Keir Starmer.

Kabla ya kuapishwa, Rais mteule Trump na makamu wa rais mteule JD Vance, watafanya kazi na timu yao ya mpito kuandaa makabidhiano hayo kutoka kwa utawala wa Rais Biden.

Walianza kubainisha vipaumbele vyao vya sera, kuanza kuhakiki wagombeaji ambao watachukua majukumu muhimu katika utawala mpya, na kujiandaa kuongoza serikali.

Trump na timu yake pia walianza kupokea taarifa za siri za usalama wa taifa zinazohusu vitisho vya sasa na operesheni zinazoendelea za kijeshi.

Rais mteule na makamu wake pia wanapata ulinzi wa lazima kutoka kwa idara ya huduma ya usalama (Secret Service) ya Marekani.

Aidha, anayeondoka kwa kawaida humwalika rais mteule katika Ikulu siku chache baada ya uchaguzi.

Pia kwa kawaida huhudhuria hafla ya uapisho wake kuashiria makabidhiano ya madaraka kwa amani, ingawa Trump aliamua kususia hafla hiyo mwaka 2020.

Hata hivyo alifuata desturi iliyoanzishwa na Ronald Reagan ya kuacha barua iliyoandikwa kwa mkono katika Ofisi ya Oval, ili mrithi wake aisome.

Wakati huo, Rais Biden aliwaambia waandishi wa habari kwamba mtangulizi wake alikuwa ameacha "barua ya ukarimu sana".

***MITANDAO***



## Halmashauri kudhibiti ubadhirifu kwa NeST

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MAOFISA masuuli, wakuu wa idara na vitengo wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida wametakiwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) kudhibiti upotevu wa fedha za serikali.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Justice Kijazi wakati wa mafunzo ya mfumo huo yanayowashirikisha maofisa, wakuu hao wa idara na vitengo.

Kijazi, alisema watumishi wanaohusika na mchakato wa ununuzi ndani ya taasisi wanapaswa kupata mafunzo ya kutumia mfumo wa manunuzi kwa ufasaha ili kudhibiti ubadhirifu huo na kuisababishia hasara ya mamilioni ya fedha za serikali.

Mkuu wa Idara ya Manunuzi wa Halmashauri hiyo, Mariam Haroun, alisema ni wajibu wa kila mtumishi wa ofisi ya manunuzi kuhakikisha anajifunza NeST na kujisajili ili kurahisisha huduma za manunuzi kwa mtandao.

Washiriki wa mafunzo hayo, walisema yatakuwa muarobaini wa upotevu wa fedha za serikali kwa kufanyika kwa NeST.

NEST ni mfumo wa elektroniki wa ununuzi wa umma ulioanzishwa na Serikali, unasisitiza uwazi katika ununuzi kuanzia kutangaza zabuni hadi kutekeleza mikataba.

Mfumo huo unaisaidia serikali kudhibiti rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma, kuchukua muda mfupi kutekeleza michakato yote ya ununuzi, kupunguza gharama na muda.

# Vijana wahamasishana kusaka ajira mitandaoni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANUFAIKA wa mradi wa Jenga Kesho Iliyobora (BBT) wamewataka vijana wenzao nchini kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali mitandaoni kujiinua kiuchumi badala ya kukaa vijiweni kusubiri ajira.

Wito huo umetolewa na Arafa Makasi, Mkazi wa Chamwino mkoani hapa, miongoni mwa wanufaika wa mradi huo katika shamba la Ndogoye lililopo wilayani Chamwino.

Arafa, alisema vijana wanapaswa kuweka utaratibu wa kutumia mitandao kufuatilia fursa hizo zinazotangazwa na serikali katika sekta mbalimbali hususani kilimo na ufugaji kujiajiri baada ya kuwezeshwa.

"Vijana tusibweteke kusubiri ajira kutoka serikalini au kampuni binafsi, kilimo ni ajira pia ukitumia vizuri fursa ya maeneo ya kilimo uliokabidhiwa kwa ajili ya uzalishaji," alisema Arafa.

Alisema serikali imewekeza kwenye sekta ya kilimo, hivyo vijana kupitia taaluma ya kilimo na nyingine wana uwezo wa kuanzisha kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia mbalimbali badala ya kusubiri msimu wa kilimo.

Mnufaika mwingine wa mradi huo, Joseph Tito kutoka jijini Mwanza, aliipongeza serikali kwa kutoa mtaji wa maeneo ya kilimo kwa vijana na kuwasaidia kupata ajira.

Tito alitaja changamoto kubwa kwa vijana wengi kuwa ni kukosa mtaji kwa ajili ya kuendeshsa kilimo cha kisasa cha mazao mbalimbali yakiwemo ya bustani.

Alisema katika shamba la Ngogoye, kila kijana atakabidhiwa ekari 10 kuzalisha mbegu bora 3 za mahindi aina ya C 105 kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

"Tunaishkuru serikali kwa kutoa fursa za kilimo kwa vijana, imesaidia kwa kiasi kikubwa kuinua kiuchumi kundi hilo," alisema Tito

Vijana hao wa awamu ya pili wa BBT, wanatarajia kuzalisha tani zaidi 8,400 za mbegu bora ya mahindi aina ya C105 katika shamba la ukubwa wa ekari 4,200 la Ndogoye wilayani Chamwino baada ya kukabidhiwa na

Mkurugenzi Msaidizi Mipango na Bajeti wa Wizara wa Kilimo, Mohamed Chikawe.

Chikawe, alisema katika shamba hilo, wanatarajia kupokea vijana 420 kwa kila mmoja kukabidhiwa ekari 10 kwa uzalishaji wa mbegu hizo za mahindi.

Alisema mbegu hizo zitakuwa bora kwa sababu zitazalishwa chini ya usimimazi wa wataalam wa kilimo.

# Wasimamizi IPOSA wanolewa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Mji Kondoa mkoani hapa imeanza kuwajengea uwezo wasimamizi wa mradi wa mafunzo changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu (IPOSA) ili kuwawezesha kujiajiri.

Ni baada ya kuanza kutoa mafunzo kwa wasimamizi hao kupitia Idara ya Elimu Msingi kuwawezesha kusimamia kwa weledi ufundishaji wa wanafunzi wa aina hiyo katika maeneo mbalimbali ya halmashauri hiyo.

Mfumo huo unalenga kufundisha wanafunzi wanaosoma nje ya mfumo rasmi katika fani za ufundi stadi wa ushonaji, seremala, uashi, mchudo na mapishi.

Akizungumza wakati wa kufungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kondoa, Christina Kalekezi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, aliwataka wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha wanawafundisha vyema vijana ili waweze kujiajiri baada ya kupata ujuzi.

Kalekezi, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wasimamizi hao kwa sababu wanakwenda kutoa elimu ya kujiajiri kwa vijana na kuondokana na tatizo la kuzagaa mitaani na kukaa vijiweni.

"Naomba wasimamizi mzingatie mafunzo haya ili mnapokwenda kuwasimamia vijana wanaosoma waweze kufanya vizuribaada ya kuhitimu," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, Justice Kijazi, akizungumza na maofisa masuhuli, wakuu wa idara na vitengo, wilayani humo jana, wakati wa mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo mpya wa kielektroniki wa ununuzi wa umma (NeST), unaolenga kukabiliana na ubadhirifu wa fedha za serikali. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Watakiwa kudhibiti matumizi ya baruti migodini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAGUZI wa migodi nchini wametakiwa kudhibiti matumizi ya baruti ili kuepuka madhara katika jamii.

Rai hiyo ilitolewa juzi jijini hapa na Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Mhandisi Ramadhani Lwamo wakati akifungua kikao cha kuwajengea uwezo wakaguzi hao wa migodi na baruti nchini.

Lwamo, alisema ametoa rai hiyo kutokana na ongezeko la uhitaji wa matumizi ya baruti nchini na changamoto kadhaa katika usimamizi wake.

"Udhibiti madhubuti ni muhimu, hivyo wakaguzi mnapaswa kudhibiti katika maeneo yenu kwani itakuwa ni aibu mkaguzi mgodi na baruti eneo lake mtu akapata madhara," alisema

Kwa mujibu wa Lwamo, matumizi ya baruti nchini yameongezeka kutoka wastani wa tani 3,000 kwa mwaka katika miaka ya 1990 hadi kufikia tani 26,516.07 kwa mwaka jana.

Alisema hali hiyo inachangiwa na ongezeko la shughuli za uchimbaji madini, utafiti wa mafuta na gesi asilia na ujenzi wa miundombinu nchini.

Vileile, alisema kumechochea kuongezeka kwa biashara ya baruti nchini tofauti na miaka ya nyuma.

Lwamo, alisema hadi sasa kuna zaidi ya bohari (magazine) 231, stoo 493, masanduku ya kuhifadhia baruti zaidi ya 279 zimesajiliwa kwa ajili ya matumizi migodini na maeneo ya biashara.

Awali Kaimu Mkurugenzi wa Ukaguzi Migodi na Mazingira, Hamisi Kamando, alisema matukio mbalimbali ya ajali yanayotokana na kutokuzingatiwa kwa sheria ya baruti ya Mwaka 1963, Kanuni za Baruti za Mwaka 1964 na taratibu zingine katika usimamizi wa baruti.

Mwanasheria Damian Kaseko wa Tume ya Madini, aliwataka wakaguzi migodi na baruti kusimamia sheria, kanuni na sera wanapotekeleza majukumu yao ili kuepusha migogoro na kuwa na mipaka katika utekelezaji wa shughuli zao.





# Mgogoro wa ardhi ulivyoua, kujeruhi ndugu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya watu wawili na kujeruhi wengine watano baada ya kuzuka mgogoro wa ardhi katika Kijiji cha Luhanga Wilaya ya Mbarali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Benjamin Kuzaga alisema tukio hilo lilitokea Januari 10, mwaka huu baada ya kutokea ugomvi baina ya familia ya Mzee Rafael Mjengwa mwenye hati namba MBL/420 iliyotolewa mwaka 1987 dhidi ya familia ya Mzee Malewa.

Alisema ugomvi huo umesababishwa na mgogoro wa shamba lenye ukubwa wa ekari 1050 baada ya familia ya Malewa kudai ni mali yao kwa ajili ya kilimo na kulisha mifugo kwa muda mrefu.

Alisema familia ya Mzee Rafael Mjengwa wakiwa wanaendelea na maandalizi ya kilimo katika shamba hilo, ghafla walishambuliwa na kundi la watu wapatao 15 wanaodaiwa kuwa ni wa Mzee Malewa na kusababisha mauaji hayo na majeruhi hao.

Aliwataja watu hao waliouawa kuwa ni Iddi Mjengwa (38), Mkazi wa Igurusi na Maige Jifaru (44) wa Isunura wilayani humo.

Kuzaga alisema baada ya polisi kupata taarifa za mauaji hao walifanya msako Januari 13 usiku na kuwakamata watuhumiwa hao, Kuva Zengo (25), Lukeresha Mlawa (32) na Bulanda Mathias (25), wakazi wa Kijiji cha Luhanga.

Awali akielezea tukio hilo, msemaji wa familia ya Rafael Mjengwa iliyofiwa na ndugu yao, George Zima alisema wakiwa kwenye shamba lao ulifika msafara wa pikipiki tisa, magari mawili na watu waliokuwa wamebeba majembe na kuwavamia.

Aliomba serikali kupitia Wizara ya Ardhi kushughulikia mgogoro huo ambao umedumu kwa muda mrefu kwa madai kuwa kabla ya kutokea tukio hilo la mauaji, walivamiwa zaidi ya mara tatu na familia ya Malewa.

"Tunaomba serikali itusaidie kwa sababu tatizo hili limekuwa kubwa na linatusababishia matatizo, tulishawahi kuwasilisha Kamati ya Siasa ya CCM na walitoa maagizo," alisema Mjengwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Maulid Surumbu aliwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi na badala yake wanapokuwa na migogoro wafuate taratibu kutatua.




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mtwivila, mjini Iringa, wakielekea shuleni kwa usafiri wa bajaji jana, kutokana na uhaba wa daladala katika barabara ya Mtwivila -Mkimbizi ambayo ni mbovu mabasi hayo hayapiti. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wajawazito wajifungua njiani wakisafirishwa kwa bodaboda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mtaa wa Igale Kaya ya Iyunga jijini hapa wameiomba serikali kuwajengea kituo cha afya ili kuwaondolea adha ya kwenda Hospitali ya Ifisi na wajawazito kujifungulia njiani wakisafirishwa kwa bodaboda.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Mmoja wa wakazi hao, Tabia Mwasomola, alisema baadhi ya wajawazito wamekuwa wakijifungulia njiani kwa kuchelewa kufikishwa Hospitali hiyo ya Wilaya ya Mbeya Vijiji iliyopo umbali wa kilomita 10 kutoka kwenye makazi yao kujifungua na kuhatarisha maisha yao na vichanga.

Tabu, alisema wamekuwa wakitumia bodaboda kusafiri kwenda katika hospitali hiyo kutokana barabara za eneo hilo kutokuwa rafiki kwa magari.

"Tunaomba tusaidiwe kwenye eneo letu hili tupate zahanati kwa sababu huduma hii tunaipata mbali sana, wajawazito wanasafirishwa kwa bodaboda na madhara yake wanazalia njiani," alisema.

Yekonia Nkembo, alisema wakazi wa eneo hilo wako tayari kujitolea maeneo kujenga zahanati na kuiomba serikali kuwasogezea huduma ya matibabu kuwaondolea adha ya kusafiri umbali mrefu hadi Ifisi na gharama za kukodi bodaboda.

Nkembo, alisema mtaa huo unazidi kukua kutokana na ongezeko la watu, lakini huduma za kijamii haziboreshwi ikiwamo afya na kusababisha madhara kwao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, John Nchimbi, alisema Kata ya Iyunga ina kituo cha afya kilichopo umbali wa kilomita 7.5 kutoka katika mtaa huo wa Igale, kwa mujibu wa sera za afya hairuhusiwi kujenga zahanati.

Nchimbi, alisema sera ya afya inataka zahanati kujengwa kwenye eneo linaloanzia umbali wa kilomita 10 kutoka kilipo kituo cha afya na kuwataka wakazi hao kuwa wavumilivu wakati malalamiko yao anatarajia kuwasilishwa kwenye vikao vya halmashauri.

Hata hivyo, aliwataka wakazi hao waendelee kutafuta eneo ili endapo taratibu zitakubalika wajengewe zahanati hiyo.

"Katika jiji letu kuna kata bado hazijawa na vituo vya afya, lakini wenzetu Iyunga wanacho kituo, sasa kwa mujibu wa sera ni kwamba hawa watu hawana sifa za kuwa na zahanati lakini kwa sababu mimi sio mwamuzi wa mwisho nalipeleka kwenye vikao vya halmashauri ili likajadiliwe," alisema Nchimbi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliagiza vikao vya kujadili malalamiko ya wakazi hao kufanyika haraka ili kufikia mwafaka.

Homera, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na nyingine muhimu kwa ustawi wa jamii.

## Wagonjwa kipindupindu wafikia 340

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDADI ya wagonjwa wa kipindupindu imeongezeka jijini hapa na kufikia zaidi ya 340 kutokana na ulaji wa vyakula visivyokuwa salama kwenye mikusanyiko ya misiba.

Ofisa Afya wa Jiji la Mbeya, Odas Aron alisema juzi pekee walipokea wagonjwa 16 kutoka maeneo ambayo awali takwimu za mlipuko huo zilikuwa zimeanza kushuka.

Aron, alisema baada ya kufuatilia historia ya wagonjwa hao, walibaini wamekula vyakula kwenye misiba, licha ya serikali kupiga marufuku mikusanyiko ya aina hiyo na ulaji wa vyakula kwenye maeneo hayo.

Alisema vyakula vingi vinavyoandaliwa kwenye misiba vinakuwa si salama kutokana na uchafu na maji yanayotumika usafi wake wa mashaka.

"Tumejaribu kupiga marufuku mikusanyiko na ulaji wa vyakula kwenye misiba lakini watu wamekuwa wabishi kwa sababu ni utamaduni wao," alisema.

Aliwataka wakazi wa jiji hilo kubadilika kwa kuacha kula ovyo, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara kwa kuwa hali ya ugonjwa ni mbaya katika maeneo yao.

**Aron, alisema baada ya kufuatilia historia ya wagonjwa hao, walibaini wamekula vyakula kwenye misiba, licha ya serikali kupiga marufuku mikusanyiko ya aina hiyo na ulaji wa vyakula kwenye maeneo hayo.**



## Wafanyakazi wahimizwa kuzingatia afya kazini

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wapya wametakiwa kuzingatia usalama wa afya zao kazini badala ya kutanguliza mishahara minono na maslahi mengine.

Mkufunzi Suleiman Khamis Ali kutoka Idara ya Usalama na Afya Kazini akitoa mada kwa watumishi wapya wa taasisi mbalimbali visiwani hapa, alisema mfanyakazi hatakiwi kusahau kulinda usalama na afya yake na ndivyo vinavyompa uwezo wa kuwajibika.

Akiwasilisha mada katika siku ya mwisho ya mafunzo yanayoandaliwa na Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) Tunguu, mkufunzi huyo, alisema majukumu ya mtumishi ni pamoja na kufanya kazi kwa ufanisi, kuchunga usalama, afya yake, ya wafanyakazi wengine, vifaa na sehemu anayotumika.

Alisema mbali na mambo mengine ya msingi ambayo mfanyakazi anawaza atapata akiwa kazini, pia asisahau kufikiria binafsi anaweza kupatwa na nini na jukumu lake katika suala hilo.

Alisema pamoja na kuwa makini na afya yake, majukumu mengine ya mfanyakazi ni kuchunga usalama wa kinachozalishwa, malighafi inayotumika na kuifahamu vyema sehemu ya kazi na taratibu zote za kiusalama na kiafya.

"Aidha awe tayari kuripoti suala la dharura la kiusalama au kiafya, kuomba na kutoa msaada inapotokea dharura yoyote inayohusiana na mambo hayo," alisema Ali.

Akizungumzia utawala, alisema unawajibika kuwakinga wafanyakazi, waajiri na jamii inayozunguka kutokana na ajali, maumivu na maradhi yatokanayo na mazingira hayo.

Alilitaja jukumu jingine kuwa ni kulinda vifaa na mitambo ya sehemu ya kazi isiharibike na kusababisha madhara kwa wafanyakazi na jamii kwa kuzorotesha uzalishaji.

Mkufunzi huyo alisisitiza kuwa mambo hayo ni lazima yashirikishe wahusika wote na yasiwe siri.

Akifunga mafunzo hayo, Mkuu wa Divisheni ya Mafunzo Elekezi na Wastaafu, Zakia Daudi Khamis, taaluma waliyopata ina umuhimu mkubwa katika mustakbali wa maisha ya wafanyakazi.

Zakia, aliwataka washiriki hao kuwa watumishi bora kwa kuwa wao ndio watendaji wakuu wa taasisi katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya taasisi na taifa.

Hata hivyo, aliwataka wakiwa kazini wasiwe na tabia mbaya, utukutu na kutafuta visingizio kukwepa majukumu, hali inayoweza kuwachafulia majalada yao.

# Baraza la Wawakilishi lawabana MaRC Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Machano Othman Said amewataka wakuu wa mikoa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mikoa miwili ya Pemba ili kukifungua kisiwa hicho kiuchumi na uwekezaji.

Machano, alitoa kauli hiyo kisiwani humo wakati akizungumza na wakuu wa mikoa hiyo, wilaya na watendaji wengine.

Alisema Serikali ya Zanzibar imedhamiria kufikisha maendeleo kisiwani humo kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi.

Alisema zaidi ya miradi 20 imewekezwa katika kisiwa cha Pemba na kuanza kutekelezwa, hivyo ni vizuri wafuatilie ili ilingane na thamani halisi ya fedha.


Machano, alisema Serikali inajenga Uwanja wa Ndege wa Pemba ili kufungua fursa ikiwemo utalii, uwekezaji na ujenzi wa Bandari ya Mkoani na meli kutoka Ulaya na nchi za Uarabuni kuanza kutia nanga na kushusha shehena za bidhaa.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea na ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini katika kisiwa hicho ili kuendelea kujiongezea mapato kupitia sekta ya usafiri wa maji.

"Kamati yetu imeridhishwa na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Kisiwa cha Pemba, wakuu wa mikoa mkiwa watendaji wakuu mnatakiwa kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo kikamilifu," alisema Machano.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema wanafuatilia miradi iliyowekezwa na kutekelezwa katika kisiwa hicho ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati na ubora kulingana na fedha zilizotolewa na serikali.

Khatib, aliipongeza serikali kwa kutekeleza miradi mingi ikiwemo ya ujenzi wa barabara na bandari kwa lengo la kukifungua kisiwa hicho kiuchumi na uwekezaji.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Balozi wa Tanzania nchini Nigeria, Celestine Kakele, alipofika Ikulu Zanzibar jana, kwa mazungumzo na kumuaga akielekea katika kituo chake cha kazi nchini humo. **PICHA: IKULU**

## Serikali kuuza kahawa mnyororo wa thamani nje

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amesema serikali imeweka mkakati kuuza nje ya nchi kahawa ilioongezewa mnyonyoro wa thamani ili kuepuka kupoteza mapato kwa kuuza kahawa ghafi.

Bashe alisema hayo leo jijini hapa wakati wa uzinduzi wa Maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Tatu wa Kahawa wa nchi 25 za Afrika zinazozalisha zao hilo na ununuaji.

Alisema katika kipindi cha miaka 10 ijayo, asilimia 50 ya kahawa inayozalishwa Afrika, ikiwemo Tanzania, serikali itahakikisha inaongezwa thamani na kuuzwa kwa matumizi badala ya kahawa ghafi na kuongeza kipato cha wazalishaji wa zao hilo.

Bashe, alisema mipango hiyo inakwenda sambamba na ujenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kahawa kwa nchi za Afrika mkoani Kilimanjaro kwa kushirikiana na Taasisi ya Uzalishaji Kahawa Afrika (IACO).

Alisema makubaliano ya ujenzi wa kituo hicho yalifanyika katika Mkutano Mkuu wa nchi za Afrika zinazolima kahawa uliofanyika hivi karibuni katika Jiji la Nairobi, Kenya.

"Tumejipanga kuhakikisha zao la kahawa linaongezwa mnyororo wa thamani na kuwainua kiuchumi wakulima nchini," alisema.

Akizungumzia kuhusu mkutano huo wa tatu Kahawa wa Nchi za Afrika uliopangwa kufanyika kuanzia Februari 21, 22, mwaka huu jijini Dar es Salaam, alisema mgeni rasmi anatarajia kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Bashe, alisema lengo la Tanzania kuomba uenyeji wa mkutano huo ni kutaka kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kahawa nchini, duniani na kushawishi wakulima kujikita katika kilimo hicho.

Alisema mutano huo ni muhimu kwa Tanzania ikizingatiwa serikali imewekeza fedha nyingi kwenye sekta kilimo ili kuinua uchumi wa nchi hasa katika mazao ya kimkakati.

Akizungumzia kuhusu uzalishaji wa kahawa nchini, Bashe, alisema umeongezeka kutoka tani 34,000 hadi kufikia 85,000 kwa mwaka jana.

Alisema hatua hiyo ni kubwa kwa kilimo cha zao hilo nchini na kuwataka wakulima kuchangia ili wazidi kukuza uchumi wao.

"Serikali iko katika hatua za kuliongezea mnyororo wa thamani ndio maana imeandaa mkutano huo wadau wa Sekta ya Kahawa kuja kubadilisha mawazo kuhusu zao hilo, pia kuona umuhimu wa biashara hiyo duniani, " alisema Waziri huyo wa Kilimo.

Alisema mauzo ya kahawa nchini yameongezeka hadi kufikia dola za Marekani 230 kutoka 140 na kukuza pato la mkulima na taifa kutokana na fedha za kigeni.

Bashe alisema hatua hiyo inaonyesha jinsi zao hilo linavyopanda thamani kila kukicha.

Alisema uzalishaji wa kahawa kwa duniani ni dola za Marekani bilioni 500, Afrika bilioni 2.5 kutokana na kuuza nje ya kahawa ghafi.

Kuhusu ujenzi wa kituo cha utafiti Kilimanjato, alisema walikubaliana na Taasisi ya IACO kutoa eneo na kuiomba kushirikiana ili kuhakikisha kahawa inayozalishwa Afrika ikiwamo Tanzania inakuwa safi na kukabiliana na ushindani katika soko la ndani na dunia.

Kwa mujibu wa Bashe, pia wanatarajia kujenga kituo cha mafunzo kwa wadau wa kahawa mtaani kwa wauzaji na wengine ili wajue umuhimu wa zao hilo.



Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maadhimisho ya miaka 60 tangu kuanzishwa kwa chuo hicho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Halmashauri tano hatari kwa matende, mabusha zatangazwa

**Na Pilly Kigome**

WAKATI serikali ikiendesha kampeni ya kutokomeza magonjwa ya matende na mabusha (ngirimaji), imeelezwa kuwa halmashauri tano nchini bado zimeendelea kuathiriwa zaidi na maambukizi ya magonjwa hayo.

Ofisa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele (NTDCP) kutoka Wizara ya Afya, Anna Joseph, alizitaja halmashauri hizo kuwa ni Kinondoni, Mtwara Mikindani, Lindi, Manispaa, Mtama na Pangani.

Joseph alitoa takwimu hizo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusema kati ya halmashauri 119 ni halmashauri 114 tu ambazo zimefanikiwa kutokomeza maambukizi ya magonjwa hayo.

Alisema kutokana na maambukizi hayo, serikali kupitia Wizara ya Afya imeandaa mkakati wa kuanza kuzifikia halmashauri hizo zilizoathirika na maambukizi kwa kuanza kutoa kingatiba kwa wananchi na wataanza na Halmashauri ya Kinondoni.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kinondoni, Dk. Peter Nsanya, alisema kwa halmashauri hiyo wataanza ugawaji kingatiba kuanzia Januari 22 hadi 26, mwaka huu katika kata 10 ambazo zimekuwa korofi katika kata 20 za eneo hilo.

Alizitaja kata hizo kuwa ni Kigogo, Mzimuni, Magomeni, Ndugumbi, Tandale Kijitonyama, Kinondoni, Hananasif, Mwananyamala na Makumbusho. Alisema kati ya kata hizo, Tandale bado ni tatizo kwa kuwa ina maambukizi ya asilimia 2.3 ukilinganisha na zingine.

Dk. Nsanya alisema katika mchakato huo wanatarajia kuwafikia wananchi wapatao 284,036 ambapo walengwa ni wenye umri wa miaka mitano na kuendelea.

Alisema kampeni hiyo ya ugawaji kingatiba itafanyika nyumba kwa nyumba, kwenye mikusanyiko, shuleni, vituo vya usafiri, masoko pamoja na kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mratibu wa miradi ya kuondoa magonjwa ya matende na mabusha kutoka Ofisi ya Mkoa Dar es Salaam, Alex Mkamba, alisema kazi ya ugawaji kinga tiba ilianza mwaka 2019 na haina madhara kwa mtumiaji.

Alisema mtumiaji wa kinga hiyo anaweza kumeza kabla au baada ya kula na haina athari yoyote.

Pia alisema kwa mwaka 2022-2023 waliwagundua wagonjwa 1,200 ambao walifanyiwa upasuaji wa kuwaondoa changamoto hiyo.

# DC afariki dunia, Samia atuma rambirambi

**Na Joyce Lameck**

MKUU wa Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Ester Mahawe, amefariki dunia.

Taarifa iliyotolewa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohammed Mchengerwa, ilisema Mahawe alifariki dunia jana katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) mkoani Kilimanjaro alikokuwa akipatiwa matibabu.

"Waziri Mchengerwa anatangaza kifo hicho kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, pia anatoa pole kwa familia, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, wafanyakazi na wananchi wote wa Wilaya ya Mbozi, ndugu, jamaa na marafiki kwa msiba huo," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Pia taarifa hiyo ilisema Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe kwa kushirikana na familia, inaendelea kuratibu shughuli za mazishi na taarifa zaidi zitaendelea kutolewa.

Wakati huo huo, Rais Samia Suluhu Hassan ametuma salamu za rambirambi kwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo kutokana na kifo hicho.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Sharifa Nyanga, ilisema Rais Samia anawapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Mahawe.

# Atangaza kiama kwa wazazi

**Na Steven William, NACHINGWEA**

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, ametangaza kufanya msako wa nyumba kwa nyumba dhidi ya wazazi na walezi ambao watashindwa shuleni.

Moyo alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhu akiagiza kwamba watoto waliochaguliwa kuanza elimu ya awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza wapelekwe shuleni na kuanza masomo mara moja.

Alisema kwa sasa wanafanya tathmini ya watoto waliojiunga na madarasa hayo na kwamba baada ya hapo wataanza kuchukua hatua ikiwamo kufanya msako nyumba kwa nyumba kuwatafuta wazazi na walezi waliokaidi kutekeleza agizo hilo.

**KUPOTEA KWA VYETI**



**RESPICIUS RICHARD MUTAGURWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S 3491-0089** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BUKOBA LUTHERAN SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017, Cheti cha chuo chenye **No. D250016** Kilichotolewa na Chuo cha **TUMAINI DAR ES SALAAM COLLEGE** mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/ILA/167659/2024**

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**MKUMBUKWA MASHA SHIDA**
Anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria (passport) yenye namba **TAE481449,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **KGT/RB/3999/2024**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**IBRAHIM H SHAIBU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S2537-0205.** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ILALA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/ILA/4127/2025**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**ABDALLAH MOHAMED ALLY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 550 ATM** aina ya **TOYOTA COROLLA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/11658/2025**

**KUPOTEA KWA VYETI**



**EVARIST ELIGI MASSAWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index **No. S1278-0132** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MBEZI HIGH SCHOOL mwaka 2014, Cheti cha DIPLOMA CLINICAL MEDICINE chenye index NS. **1278/0132/2014** Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **CITY COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCE** mwaka 2023. . Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/259347/2024**

**TANGAZO!! TANGAZO!!**
**MNADA WA HADHARA WA NYUMBA**

**FAGIO BROKERS AND AUCTIONEERS CO.LTD**
Kwa amri tuliyopewa na baraaza la ardhi na Nyumba Mbeya, tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba moja mali ya Yohana Levi Ngogo iliyopo mtaa wa Nyibuku kata Mwakibete (Mabanzini), Mkoa wa Mbeya.
Mnada utafanyika tarehe 23/01/2025 mahali nyumba ilipo kuanzia saa 5:00 kamili asubuhi.

**MASHARTI YA MNADA:**
1. Mshindi atalipa 25% ya bei ya mali aliyonunua na kiasi kitakacho baki kitalipwa ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya mnada.
2. Gharama za kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.

**MAWASILIANO: 0768224862/0754446937**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**GABRIEL MARIK NGOWI**
ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA STARLET YENYE USAJILI NO **T348 AKJ.** CHASSIS NO **EP910031347.** ENGINE NO 4E1713988. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA KUTOA TAARIFA KITUO CHA POLISI.
**AR/RB/12334/2024**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**GOODLUCK LUCAS MBILINYI**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.927 CFA** AINA YA SUZUKI CARRY. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.
TAARIFA YA POLISI
**PHQ/MBE/MBE/1832/2025**

# Kenya yakanusha Raila kujiondoa kinyang'anyiro AU

**NAIROBI, Kenya**

KENYA imesema Waziri Mkuu wa zamani Raila Odinga yuko katika kinyang'anyiro cha kumrithi Moussa Mahamat wa Chad kama mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AU) huku kukiwa na uvumi kwamba Odinga alikuwa akifikiria kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Ripoti, ambazo vyanzo vyake havikufahamika mara moja, ziliibuka jana zikieleza kuwa Odinga, angejiondoa huku kukiwa na upungufu uliotabiriwa wa kura za kumfanya ashinde Februari mwaka huu.

Odinga anakabiliwa na wagombea wengine wawili, huku Waziri wa Mambo ya Nje wa Djibouti Mahamoud Ali Youssouf, akisemekana kuwa mpinzani wake mkuu, pamoja na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Madagascar Richard James.

Ofisa mkuu wa serikali ya Kenya, ambaye aliomba kutotajwa jina, aliiambia TRT Afrika kuwa sio kweli kwamba Odinga alikuwa anafikiria kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha uenyekiti wa Tume ya AU.

"Yeye Odinga hataondoka katika kinyang'anyiro. Anashinda," ofisa huyo mkuu, ambaye ni mwanachama wa watendaji wakuu wa Rais William Ruto, alisema kwa kujiamini jana.

Vyanzo vingine ndani ya serikali pia vilikanusha taarifa kwamba Odinga alikuwa akifikiria kujiondoa kwenye kinyang'anyiro cha uenyekiti wa Tume ya AU.

Wakati huo huo, waziri mkuu wa zamani wa Kenya, ambaye alihudumu kutoka 2008 hadi 2013, alimtembelea Rais wa Zimbabwe Emmerson Mnangagwa mjini Harare juzi kutafuta uungwaji mkono kwa azma yake ya AU.

"Imekuwa furaha kujumuika na rais Mnangagwa maono yangu kwa Afrika na kujadili kugombea kwangu uenyekiti wa AU," Odinga alisema kwenye mtandao wa X.

Akizungumza baada ya kukutana na Rais Mnangagwa, Odinga alisema atazuru mataifa mengine katika eneo la Kusini mwa Afrika kutafuta uungwaji mkono kwa azma yake ya kuwa mwenyekiti wa Tume ya AU.


"Rais wa Zimbabwe ndiye mwenyekiti wa sasa wa kambi ya kanda ya Kusini mwa Afrika (SADC). Hivyo ilikuwa muhimu kwangu kuja Harare," Odinga alisema.

"Tumebadilishana mawazo na ndugu yangu Rais Mnangagwa, tunajua tunakotoka, na tunajua tunakotaka kwenda, Afrika ina mustakabali mzuri, lakini Afrika itaendelezwa na Waafrika wenyewe tu. ili kupata pesa, haziji kuendeleza Affika ni lazima tuwe na dira ya wazi ya jinsi ya kuendeleza Afrika," Odinga alisema.

Inaelezwa kuwa mwenyekiti wa Tume ya AU anachaguliwa na wakuu wa nchi za Afrika kupitia kura ya siri kwa muhula wa miaka minne, unaoweza kuongezwa mara moja, na kwamba mshindi wa nafasi hiyo lazima apate kura zisizopungua theluthi mbili, ambayo ni 36 kati ya zaidi ya kura 50.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa waziri mkuu wa zamani wa Chad na mwenyekiti wa sasa wa Tume ya AU, Moussa Mahamat, 64, amemaliza muda wake wa uongozi.

*TRT*



Waziri Mkuu wa zamani wa Kenya, Raila Odinga (kushoto) akisalimiana na Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa mjini Harare, baada ya kumtembelea jana. **PICHA: MTANDAO.**

# Ripoti: Trump asingeshinda angehukumiwa

**NEW YORK, Marekani**

RIPOTI ya idara ya sheria iliyotolewa kwa Bunge nchini Marekani imebainisha kwamba Rais mteule Donald Trump angehukumiwa kwa kujaribu kubadilisha matokeo ya uchaguzi wa urais wa 2020 ambayo alishindwa ikiwa hangefanikiwa kuchaguliwa tena 2024.

Ripoti hiyo ya wakili maalum Jack Smith iliyotolewa jana ilieleza kuwa ushahidi unaokubalika pasi na shaka ulitosha kumfungulia mashtaka kiongozi huyo mteule wa kiti cha urais.

Ilielezwa kuwa ripoti hiyo ilipomfikia Trump saa chache baada ya kutolewa alikanusha vikali akisema "Smith amechanganyikiwa na matokeo yake ni feki".

Ilibainishwa kuwa nyaraka hiyo ya kurasa 137 ilitumwa kwa Bunge baada ya Jaji Aileen Cannon kuruhusu kutolewa kwa sehemu ya kwanza kati ya mbili za ripoti ya Smith kuhusu kesi ya kuingiliwa kwa uchaguzi.

Aliamuru kusikilizwa kwa kesi nyingine baadaye wiki hii kuhusu kutolewa kwa sehemu ya ripoti juu ya madai kwamba Trump alihifadhi hati za serikali kinyume cha sheria.

Aidha, ilielezwa kuwa wakili Smith alijiuzulu kutoka wadhifa wake wiki iliyopita. Baada ya kuhudumu katika nafasi hiyo tangu 2022 katika kusimamia uchunguzi wa Idara ya Sheria ya Marekani juu ya Trump.

Mawakili maalum huchaguliwa na idara katika kesi ambapo kuna uwezekano wa mgongano wa maslahi.

Trump alishtakiwa kwa kuhifadhi hati kinyume cha sheria na, katika baadhi ya kesi, kuzihifadhi katika vyumba vya mapumziko ya Mar-a-Lago huko Florida, kwenye makazi yake.

Katika kesi ya uingiliaji kati uchaguzi, alishtakiwa kwa kula njama ya kutengua matokeo ya uchaguzi wa 2020.

Kesi zote mbili zilisababisha mashtaka ya jinai dhidi ya Trump, ambaye alikanusha kuwa na hatia na kudai kuwa yaliyochochewa kisiasa.

Lakini Smith alifunga kesi hizo baada ya Trump kushinda uchaguzi mwezi Novemba, kwa mujibu wa kanuni za Idara ya Sheria zinazokataza kufunguliwa mashitaka kwa rais aliye madarakani.

*BBC*

## Moshi mweupe waonekana usitishaji vita Gaza

**GAZA, Palestina**

WAPATANISHI wa Marekani na mataifa ya Kiarabu wamepiga hatua kubwa kuelekea kupatikana kwa makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya Israel na kundi la Hamas na kuachiliwa kwa mateka wanaoshikiliwa katika Ukanda wa Gaza.

Maofisa wanne ambao ni wajumbe wa baraza la upatanishi walisema jana kwamba siku zijazo zitakuwa na umuhimu mkubwa kuelekea kupatikana kwa makubaliano ya kusitisha vita vya zaidi ya miezi 15 ambavyo vimevuruga eneo la Mashariki ya Kati.

Maofisa hao wamezungumza kwa masharti ya kutotajwa majina kwa sababu hawajaruhusiwa kujadili kuhusu mazungumzo hayo yanayofanyika mjini Doha, Qatar.

Ofisa mmoja wa Marekani anayefahamu kwa undani juu ya mazungumzo hayo alisema, pande zote ziko karibu zaidi kufikia makubaliano, lakini ametahadharisha kuwa bado hali inaweza kubadilika wakati wowote.

Ofisa huyo alikataa kutoa utabiri juu ya wakati ambao makubaliano hayo yanaweza kufikiwa akisema kuna hali isiyoeleweka, na vipengele vingi bado havijakamilika.

Mara kadhaa katika kipindi cha mwaka uliopita, viongozi wa Marekani walieleza matumaini kwamba, walikuwa karibu kufikia makubaliano ya kusitisha mapigano, ingawa baadaye mazungumzo hayo yalikwama.

Pia ofisa mwengine alieleza kuwa kumekuwepo dalili ya kufikia makubaliano na tayari lipo pendekezo kwenye meza ya mazungumzo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa, wajumbe wa Israel na Hamas wataliwasilisha pendekezo hilo kwa viongozi wao kwa ajili ya idhini ya mwisho.

Ofisa huyo alisema, wapatanishi kutoka Qatar wameweka shinikizo jipya kwa Hamas kukubali pendekezo hilo la kusitisha mapigano huku mjumbe wa Rais mteule wa Marekani Donald Trump, Steve Witkoff, akiishinikiza Israel kulikubali pendekezo hilo.

Witkoff hivi karibuni alijiunga na mazungumzo hayo na ameonekana katika eneo la Mashariki ya Kati mara kwa mara katika siku za hivi karibuni.

Alisema wapatanishi wamekabidhi rasimu ya makubaliano kwa kila upande huku saa 24 zijazo zikitajwa kuwa na umuhimu wa kuamua hatma ya mazungumzo hayo.

*DW*

# Beki aliyetakiwa Simba aibukia Mashujaa FC

Na Adam Fungamwango

WAKATI dirisha dogo la usajili likitarajiwa kufungwa leo saa 6:00 usiku, huku klabu mbalimbali zikiwa kwenye pilikapilika ya kukamilisha uhamisho wa wachezaji ili kuwahi muda, Klabu ya Mashujaa FC, imetajwa kukamilisha uhamisho wa mkopo wa beki wa kushoto, Yahaya Mbegu, akitokea Singida Black Stars.

Mbali na hilo, imetajwa kuwa beki wa kati ya zamani wa Simba na Yanga, Kelvin Yondani, anatarajiwa kujiunga na Ken-Gold, baada ya dili lake la awali kuichezea Pamba Jiji kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu kushindikana.

Habari kutoka ndani ya klabu ya Mashujaa, zinasema kuwa wamempata Mbegu kwa mkopo wa miezi sita, lakini kukiwa na kipengele cha kumsajili moja kwa moja kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu.

Miaka miwili iliyopita, Mbegu alikuwa akihusishwa kujiunga na Simba, lakini dili hilo lilikuwa likishindikana katika dakika za mwisho kwa misimu miwili, akiwa kwenye Klabu za Singida Big Stars na Ihefu FC.

„Tumemuongeza Mbegu, na wengine wapo, lakini ndiyo tunamalizana nao, tukishakuwa tayari kila kitu tutawatangazia, nadhani muda si mrefu kwa sasa kipindi cha usajili kimeshamalizika," kilisema chanzo hicho.

Wakati hayo yakiendelea Mashujaa FC, Klabu ya KenGold ambayo inaonekana imepania kufanya usajili mkubwa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, imekamilisha dili la kumsajili beki wa kati wa zamani wa Yanga, Yondani.

Habari zinasema kuwa beki huyo naye anatarajiwa kutambulishwa kwenye tamasha lililopewa jina la Makarasha Day, ambalo litafanyika jijini Mbeya kwa lengo la kuwatambulisha wachezaji iliyowasajili kutoka Msumbiji, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Zambia na hapa nchini, akiwamo Mghana, Benard Morrison kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Jose Mkoko.

Awali, beki huyo alikuwa kwenye mazungumzo na Pamba Jiji ambayo yalishindikana, badala yake KenGold ikachukua nafasi hiyo.

Yondani ambaye mara ya mwisho aliichezea Polisi Tanzania, hakuonekana tena uwanjani msimu huu.

# SABABU CHAN KUPIGWA KALENDA

Na Shufaa Lyimo

WAKATI droo ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) 2024, ilitarajiwa kufanyika Nairobi nchini Kenya leo, Watanzania wametakiwa kutumia vema fursa zitakazopatikana katika mashindano hayo ambayo yalitarajiwa kuanza Februari Mosi hadi 28, mwaka huu, lakini kukaibuka taarifa za kupangwa kuahirishwa.

Mashindano hayo ambayo kwa mara ya kwanza yatafanyika Afrika Mashariki kwa ushirikiano wa mataifa matatu, Tanzania, Kenya na Uganda, taarifa zinadai huenda yakaahirishwa hadi Agosti mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali zilizolifikia gazeti hili jana, sababu ya kupangwa kuahirishwa ni uhaba wa viwanja, ukosefu wa miundombinu mingine na vitendea kazi.

Kingine ni uwezekano wa kupata sti kamili ya timu 19 kwani kwa sasa zilizopo ni 17 tu, huko Shirikisho la Soka Afrika(CAF), likitaka pia kuacha kwanza hadi ligi zote za ndani Afrika zimalizike kwanza.

Kadhali, kutaka kutoa nafasi kwa kwa mataifa mengine kama Algeria, Misri na Afrika Kusini kujiandaa kwa mechi za mtoano kupata timu zitakazoongezeka kukamilisha seti ya timu 19 shiriki kwenye michuano hiyo ya CHAN.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya CHAN 2024 na AFCON 2027, Leodgard Tenga, ndiye aliyetoa wito huo kwa Watanzania kujiandaa kutumia fursa kwenye michuano hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea maandalizi ya mashindano hayo kabla ya Nipashe kudokezewa taarifa ya kupangwa kuahirishwa.

"Ninaomba Watanzania watumie vema fursa zao pindi mashindano hayo yatakapoanza hata yatakapofika yale ya AFCON yatakayofanyika mwaka 2027 kwa ushirikiano wa nchi ya Kenya na Uganda ili waendelee kukumbuka huduma zetu," alisema Tenga.

Mwenyekiti huyo alisema kamati yake imeliomba Shirikisho la Mpira wa Miguu barani Afrika (CAF), kuweka viingilio rafiki ili kila mmoja aweze kuingia uwanjani.

Alisema serikali imefanya ukarabati wa miundombinu ya viwanja kwa ajili ya mashindano hayo ambayo inaendelea kufanyika ikiwamo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa pamoja na ule wa New Amaan Complex uliopo visiwani Zanzibar.

Vile vile alisema mbali na viwanja hivyo, pia ukarabati unaendelea kwenye viwanja vitakavyotumika kufanyia mazoezi ambavyo ni Gymkhana, Law School na ule wa Meja Jenerali Isamuyo, ambapo mpaka sasa ukarabati huo umefikia asilimia 95.

Aidha, alisema timu zote zitaanza kuwasili nchini kati ya Januari 24 na 25, mwaka huu, na kudai ni wakati wa kuwatangaza wachezaji wetu kupitia mashindano hayo.

"Wageni wataanza kuwasili hapa nchini wiki moja kabla ya kuanza mashindano ili wahakikishe hoteli huku wakiambatana na wawakilishi kutoka Fifa na CAF," alisema Tenga.

Alisema katika mwendelezo wa maandalizi ya mashindano hayo wameandaa kongamano la wadau mbalimbali wa michezo litakalofanyika leo kwenye Ukumbi wa Johari Rotana jijini Dar es Salaam, lenye lengo la kutoa taarifa kwa hatua waliyofikia mpaka sasa.

Tenga alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, Dk. Samia Suluhu Hassan, kutokana na juhudi kubwa anazozifanya kuhakikisha nchi yetu inafika mbali kwenye sekta ya michezo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya CHAN 2024 na AFCON 2027, Leodgard Tenga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuelekea maandalizi ya michuano ya CHAN itakayoanza kutimua vumbi Tanzania, Kenya na Uganda, kuanzia Februari Mosi hadi 28, mwaka huu. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Simfukwe atoboa siri wimbo wa Chanzo

Na Mwandishi Wetu

MWANAMUZIKI maarufu wa Muziki wa Injili nchini, Rehema Simfukwe, amevunja ukimya kwa mara ya kwanza kwa kuamua kutoa sababu za kutunga wimbo wa ‚Chanzo' ambao umekuwa ukipendwa na kuvuta hisia za watu wengi kutokana na mashairi yaliyoandikwa katika wimbo huo.

Simfukwe tangu alipotoa wimbo huo miaka minne iliyopita, hakuwahi kutoa sababu za kutunga na kuimba wimbo huo, lakini ameona sasa ni wakati muafuaka kuwaambia Watanzania kuhusu wimbo Chanzo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati wa hafla fupi ya kuelezea sababu za kuimba wimbo wa Chanzo, Simfukwe alisema, mtoto wake (Dorcas) ndio sababu iliyomfanya yeye kuimba wimbo huo kwani alimzaa na amekuwa na changamoto ya kupooza kwa ubongo (mtindio wa ubongo)

"Mungu amenijaalia watoto watatu, lakini duniani huku watu wengi wanajua nina watoto wawili. Mtoto wangu wa kwanza anaitwa Dorcas ambaye alizaliwa na changamoto ya kupooza ubongo au mtindio wa ubongo kwa hiyo alikuwa na changamoto sana katika maisha yake

"Changamoto hiyo kwa Dorcas ilisababisha tangu alipozaliwa tukawa na maisha ya hospitalini siku hadi siku. Nimekuwa nikiimba nyimbo za injili, nafanya mahojiano na vyombo vya habari kuhusu wimbo wa Chanzo, lakini sijawahi kueleza upande wa pili kuhusu wimbo huu," alisema Simfukwe.

Alisema amekuwa kimya muda wote kwa sababu alikuwa anasubiri apate kibali kutoka kwa Mungu kuzungumzia wimbo huo na hiyo ndio sababu ya kutunga na kuimba wimbo huo ambao unazungumzia maisha halisi ya Mtoto Dorcas.

"Ukiusikiliza wimbo huu utaona ndani yake kuna ujumbe uliobeba maumivu ya Dorcas na ndio sababu ya kuuimba, nafahamu tangu ulipotoka watu wameuopokea, na wamekuwa wakiuimba na kuufurahia na nimekuwa nikiulizwa sababu za kuimba wimbo huu.

"Nilimuahidi Mungu kuwa sitasema hili mpaka pale atakaponiruhusu na nimekaa na hii siri kwa miaka kadhaa na ninaamini Mungu amenipa mtoto Dorcas ili niwe mfano kwa wengine, ili nisaidie wengine wenye watoto wenye changamoto kama za Dorcas.

Hata hivyo, alisema wakati wakisherehekea kumbukizi ya kuzaliwa kwa Dorcas pia ameamua kutangaza kufungua kituo cha kulea watoto ambao wanachangamoto ya mtindio wa ubongo. Kituo hicho kitafahamika kwa jina la Dorcas Home Care Initiative kilichopo Madale jijini Dar es Salaam.

"Wakati leo tunafurahia miaka sita ya Dorcas naomba nitangaze uwapo wa Dorcas Homecare Initiative, lengo la kituo hiki ni kupokea watoto wenye changamoto ya mtindio wa ubongo, na hakutakuwa na gharama yoyote kwani nimeamua kutoa huduma ya kulea watoto hao na nimeanza na watoto nane.

## ZISIKUPITE

### GARNACHO NA MAN UNITED

MANCHESTER United inasemekana kumthamininisha winga Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 20, kwa takriban pauni milioni 42, huku kukiwa na nia ya Napoli kumnyakua mchezaji huyo. ***(Sport Italia)***

### MAINOO AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich imeungana na Chelsea katika mbio za kumnunua kiungo wa kati wa Manchester United na England, Kobbie Mainoo, 19**.** ***(Sun)***

### WALKER ARUHUSIWA KUONDOKA

KLABU ya Manchester City wako tayari kumruhusu mlinzi Kyle Walker mwenye umri wa miaka 34, kuondoka bila malipo mwezi huu, huku AC Milan na Inter Milan zikionesha nia ya kumnasa mchezaji huyo. ***(Gazzetta dello Sport)***

### MILAN YAMFUATILIA RASHFORD

AC Milan itamfuatilia rasmi mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, ambaye anatazamiwa kuondoka Old Trafford mwezi huu. ***(Sky Sports)***

### DORTMUND PIA YAMTAKA

KLABU ya Borussia Dortmund pia imeripotiwa kukutana na wawakilishi wa Marcus Rashford kwa matumaini ya kumsajili Januari hii**.** ***(Sky Sport)***

### MALEN KUTUA ASTON VILLA

KLABU ya Aston Villa imekubali mkataba wa pauni milioni 19 kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 25 kutoka Borussia Dortmund. ***(Athletic)***

### COULIBALY ANUKIA LEICESTER

KLABU ya Leicester City inajiandaa kumsajili mlinzi wa pembeni wa Ufaransa, Woyo Coulibaly mwenye umri wa miaka 25, kutoka Parma kwa mkataba wa pauni milioni 3. ***(Fabrizio Romano)***

### CHUKWUEMEKA KURUHUSIWA

CHELSEA itamruhusu kiungo, Carney Chukwuemeka mwenye umri wa miaka 21, kuondoka kwa mkopo mwezi huu, huku Borussia Dortmund na Strasbourg zikimwania. ***(Fabrizio Romano)***

### FORES KUPOKEA OFA

KLABU ya Nottingham Forest iko tayari kupokea ofa kwa ajili mshambuliaji, Emmanuel Dennis, 27. ***(Sky Sports)***

### VEIGA KUONDOKA CHELSEA

MLINZI wa Ureno, Renato Veiga mwenye umri wa miaka 21, ana uwezekano wa kuondoka Chelsea Januari hii, huku klabu za England, Ujerumani, Ufaransa na Italia zikionesha nia ya kumtaka. ***(Athletic)***

### ALVAREZ OFA YA PILI

MONACO imetoa pendekezo la pili kwa West Ham kwa ajili ya kumsajili Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 27, baada ya ofa yao ya awali ya mkopo kwa kiungo huyo wa Mexico kugonga mwamba. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA WAMTAKA ISAK KUMRITHI LEWANDOWSKI

Mashine ya mabao ya Sporting CP, Viktor Gyokeres pia anatajwa kuwa shabaha...

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA bado inapanga kumtafuta mrithi wa Robert Lewandowski, huku ripoti zikimtaja tena Alexander Isak kama mchezaji anayelengwa sana na miamba hao wa Katalunya.

Lewandowski, ambaye sasa ana umri wa miaka 36, haoneshi dalili za kupunguza kasi mbele ya lango na anaendelea kujivunia rekodi nzuri ya utimamu wa mwili.

Amefunga mabao 16 katika mechi 18 za LaLiga msimu huu na amefunga mengine tisa katika mashindano mengine na kufikisha jumla ya mabao 25.

Lewandowski alijiunga na Barcelona akitokea Bayern Munich na sasa anaonekana kwamba umri unazidi kumtupa mkono.

Isak ndiye anayeonekana kuwa anaweza kumrithi Lewandowski hasa kutokana na kiwango chake cha kuvutia kule Newcastle United, akifunga katika mechi saba za mwisho za Ligi Kuu England na kufunga bao la wastani kila dakika 113.

Jarida la Hispania la Mundo Deportivo limebainisha kwamba, Isak ambaye aliigharimu Newcastle pauni milioni 63 wakati akijiunga kutoka Real Sociedad mwaka wa 2022, ndiye anayeongoza kuchukua nafasi ya Lewandowski.

Mashine ya mabao ya Sporting CP, Viktor Gyokeres pia anatajwa kuwa shabaha kuu ya Barcelona, ingawa yeye, kama Isak, huenda akaigharimu Barcelona kiasi kikubwa cha fedha - kiasi ambacho wababe hao wa Katalunya hawana kwa sasa wanapoendelea kukabili matatizo ya kifedha.



# JESUS AZUA HOFU ARSENAL

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amekiri kuwa kuna wasiwasi mkubwa kuhusu Gabriel Jesus baada ya fowadi huyo kutolewa nje kwa machela wakati wa mechi ya Jumapili ya Kombe la FA dhidi ya Manchester United.

Jesus alianza mchezo upande wa kulia baada ya Kai Havertz kuwa kwenye kiwango bora katika michezo kadhaa ya hivi karibuni akicheza namba tisa.

Lakini Mbrazil huyo alilazimika kutolewa nje kabla ya kipindi cha mapumziko baada ya kugongana na Bruno Fernandes na kuanguka vibaya.

"Wasiwasi mkubwa. Hizo ni hisia zangu," alisema Arteta.

"Ilibidi atoke kwenye machela akiwa na maumivu. Alishika goti lake, haionekani kuwa ni nzuri."

Ubora wa Arsenal katika hatua hii ni kwamba haionekani kuwa marudio ya shida ambayo Jesus alikumbana nayo kwenye Kombe la Dunia la 2022, ambapo ilimfanya kuwa nje kwa kipindi cha miezi minne.

"Nadhani ni goti lingine. Sababu ya wasiwasi ni hisia aliyokuwa nayo. Ilibidi atoke na maumivu aliyokuwa nayo," alisema Arteta.

Tayari kulikuwa na kelele kutoka kwa mashabiki wa Arsenal kutaka kujiimarisha kwa kusajili fowadi mpya kipindi hiki cha usajili wa Januari, ambao umeongezeka baada ya jeraha la Jesus.

Bukayo Saka na Ethan Nwaneri tayari wapo nje, huku Jesus akiwa amefunga mara sita katika mechi saba zilizopita na 'Washikabunduki' hao sasa wanakosa mshambuliaji halisi wa kati.

Hata hivyo, Arteta alisema anaendelea kuwaamini na kuzingatia wachezaji ambao bado anao na kusisitiza hayuko katika udhibiti wa uwezekano wa kusajili.

"Namaanisha, tunakosa kutoka kwa njia mbalimbali, kutoka kwa michezo tofauti. Na ninaelewa hilo, lakini siwezi kuwasajili wachezaji zaidi. Na ninazingatia sana kile ambacho tunapaswa kufanya kwa kiwango cha juu," alisema.

# Neymar hatihati kutua Marekani

**MIAMI, Marekani**

KOCHA wa Inter Miami, Javier Mascherano, amesema "haitawezekana" kumsajili Neymar kutoka Al Hilal kutokana na kiwango cha ukomo wa mishahara katika Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Nyota huyo wa Brazil ameichezea Al Hilal mechi saba pekee tangu alipohamia Saudi Arabia Agosti 2023, huku jeraha la misuli likimweka nje kwa takriban mwaka mmoja.

Amepata matatizo zaidi ya utimamu wa mwili tangu arejee kwenye kikosi Oktoba mwaka jana.

Kutocheza mara kwa mara kwa Neymar kule Mashariki ya Kati kumesababisha mazungumzo ya uwezekano wa kuondoka Januari hii au majira ya joto, na amekiri kwamba angependa kuungana na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona, Lionel Messi na Luis Suarez kule Inter Miami.

Watatu hao waliunda safu bora ya ushambuliaji maarufu kama 'MSN' wakati wakicheza pamoja kule Barcelona kati ya 2014 na 2017.

Akizungumza na CNN, Neymar alikiri: "Ni wazi, kucheza tena na Messi na Suarez litakuwa jambo zuri. Ni marafiki zangu. Bado tunazungumza. Ingependeza kufufua utatu wetu.

"Nina furaha nikiwa Al Hilal, nina furaha Saudi Arabia, lakini nani anajua. Soka imejaa mshangazo, sijui nini kitatokea kesho."

Hata hivyo, licha ya matamshi ya Neymar kuzidisha uvumi juu ya kuhamia MLS, Kocha wa Inter Miami, Mascherano, ambaye alicheza na Neymar katika Klabu ya Barcelona, pia amedai kuwa hawataweza kufanya makubaliano kutokana na kiwango cha juu cha mshahara wa ligi.


"Hatuwezi kuzungumza kuhusu Ney kwa sababu hatuna chochote," alisema Mascherano mwenye umri wa miaka 40.

"Ni wazi Ney ni mchezaji mkubwa. Kila kocha duniani anamtaka, lakini kwa sasa MLS ina kikomo cha mshahara. Kwa hiyo kwetu kwa wakati huu, haiwezekani kujaribu kumfikiria."

Msimu mpya wa MLS utaanza Februari 22 na Inter Miami, ambao walishinda Ngao ya Mashariki kwa mara ya kwanza mwaka 2024, watapata fursa ya kuimarisha kikosi chao dirisha la uhamisho litakapofunguliwa mwishoni mwa Januari na litafungwa Aprili.

# Fury atangaza kustaafu ndondi

**LONDON, England**



BINGWA wa zamani wa ndondi wa uzito wa juu duniani, Tyson Fury, ametangaza kustaafu kucheza mchezo huo.

Fury alipigana mara ya mwisho Desemba mwaka jana alipopoteza pambano lake la marudiano la kuwania mikanda ya WBA na WBC na bingwa wa WBO, Oleksandr Usyk.

Fury mwenye umri wa miaka 36, hapo awali alitangaza kustaafu baada ya kumpiga Dillian Whyte Aprili 2022, lakini akarejea miezi sita baadaye.

Mwingereza huyo amefurahia nafasi mbili kama bingwa wa uzani wa juu na ana rekodi ya kushinda mapambano 34, na kupigwa mara mbili na sare moja.

"Ningependa kutangaza kustaafu kwangu kucheza ndondi, nilifurahia kila dakika na nitamalizia na hili."

Fury alimshangaza bingwa wa dunia aliyetawala mchezo huo kwa muda mrefu, Wladimir Klitschko, mwaka 2015 na kushinda mataji ya WBA, IBF, WBO na IBO.

Baada ya zaidi ya miaka miwili na nusu nje ya ulingo, ambapo alishughulikia masuala ya afya ya akili, Fury alirejea ulingoni mwaka 2018 na kuwa bingwa mara mbili kwa kumshinda Deontay Wilder na kutwaa mkanda wa WBC mwaka 2020.

# JKT QUEENS YATAMBA IPO VIZURI KUCHAPA WOTE GIFT

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la Ufundi la Timu ya JKT Queens wenye umri chini ya miaka 17, limesema halina wasiwasi kukutana na timu yoyote katika mashindano ya CAF U-17 Girls Integrated Football Tournament (GIFT), yanayoendelea katika Uwanja wa Azam Complex, Chamanzi, Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Jumatatu usiku baada ya kumalizika kwa mchezo wao dhidi ya City Lights FC ya Sudan Kusini na kushinda mabao 10-0, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Esther Chabruma, alisema amefurahishwa na ushindi walioupata licha ya kutokuwa rahisi.

„Nipo tayari kukutana na timu yoyote kwa kuwa nina matumaini makubwa na timu yangu, ninawashukuru pia mashabiki kutokana na ushirikiano wanaotuonesha tunapokuwa uwanjani," alisema Chabruma.

Akizungumzia mchezo huo, alisema waliingia wakiwa na tahadhari kuhakikisha wanapata pointi tatu jambo ambalo limewafanya wapate idadi kubwa ya magoli.

Kocha huyo alisema siri ya mafanikio yao imetokana na wachezaji wake kufuata maelezo anayowapa, nidhamu pamoja na ushirikiano waliokuwa nao.

Alisema anashukuru hana majeruhi yeyote kwani wachezaji wake wote wanaendelea vema kiafya.

Kwa ushindi huo wa mabao 10-0 dhidi ya City Lights FC, JKT Queens imefikisha pointi 9 huku ikiendelea kuongoza katika Kundi A.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa City Lights, alidai kuwa wameshindwa kufanya vizuri kutokana na wachezaji wake kuwa na umri halali tofauti na ukiwalinganisha na wapinzani wao.

"Tumeshindwa kufanya vizuri kwa kuwa tumekutana na wachezaji wenye umri zaidi ya miaka 17, hivyo waliwazidi nguvu wachezaji wangu," alisema



Kocha wa JKT Queens, Ester Chabruma

# Mpole kupelekwa Singida kwa mkopo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba Jiji iko kwenye hatua za mwisho za kumpeleka straika George Mpole Klabu ya Singida Black Stars kwa mkopo kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili leo saa sita usiku.

Taarifa kutoka ndani ya Klabu ya Pamba Jiji, zimeleza kuwa mbali na Mpole, klabu hiyo pia inatarajiwa kumpekeka straika wao mwingine raia wa Ghana, Erick Okutu kwa mkopo katika Klabu ya KenGold, ingawa mwenyewe anapinga akitaka avunjiwe mkataba kama hawataki kuendelea naye.

Chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo kimesema kuwa Pamba, inamuondoa Mpole kutokana na kutoridhishwa na kiwango chake, huku Okutu akitajwa kuwa ni mtovu wa nidhamu.

Aidha, chanzo kingine kimedai kuwa Singida Black Stars, imemuomba Mpole ili kwenda kusaidiana na Elvis Rupia kwenye safu ya ushambuliaji, wakiamini anaweza kufanya vema katika timu yao kuliko huko aliko.

Kinasema Singida Black Stars, imetumia fursa hiyo, baada ya kuwapatia Pamba Jiji, wachezaji Habib Kyombo, Hamad Majimengi na kipa Mohamed Kamara, kipa wa zamani wa Horoya FC, raia wa Sierra Leone.

"Baada ya kukamilisha usajili wa washambuliaji, Habib Kyombo na Mathew Tegisi Momanyi tumeona Mpole tumtoe kwa mkopo na Singida Black Stars imeonesha nia ya kumhitaji, lengo ni kudumisha uhusiano uliopo baina yetu," kilisema chanzo hicho.

Pamba imemsajili straika Momanyi kutoka Shabana FC ya Kenya, ambapo anatarajiwa kuwa miongoni mwa wachezaji watakaoivaa Dodoma Jiji katika mchezo wao kwa kwanza wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, itakayoanza kutimua vumbi tena kuanzia Machi Mosi, mwaka huu.

Mpole aliyejiunga na kikosi hicho msimu huu baada ya kuachana na FC Lupopo ya DR Congo, anakumbukwa zaidi msimu wa 2021/22, alipoibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu Bara akitupia mabao 17, akimuacha 'solemba', kwa tofauti ya bao moja, straika wa Yanga wakati huo ambaye kwa sasa anaichezea, Pyramids ya Misri, Fiston Mayele.

## CAF yafungia mashabiki Simba, Fadlu afunguka

INATOKA UK. 24

tika siku hizo zilizobaki za mazoezi nitakachofanya ni kuwaelekeza wachezaji wangu jinsi gani ya kukabiliana nayo. Haitokuwa CS Constantine kama ile iliyocheza ikiwa kwao nchini Algeria, tunahitaji kuwasukuma kwa nguvu langoni kwao, tunatakiwa kuwa na ubunifu, kushambulia bila kuchoka kwa ajili ya kuvunja mitego yote, kupasua ukuta waliouweka na mwishowe kuibuka na ushindi," alisema Fadlu.

Alirejea tena kauli yake kuwa ushindi katika mchezo wa Jumapili ijayo ni muhimu mno licha ya kwamba wameshatinga hatua ya robo fainali, kwani unaweza kuwa njia ya kuwarahisishia kazi kwenda kwenye hatua ambayo wanachama na mashabiki wa Simba wanaihitaji sana, nusu fainali.

"Mpango wa kwanza wa robo fainali umekamilika, wa pili ni kuongoza kundi ili tupate nafasi ya kuanzia ugenini pindi droo itakapopangwa na kumalizia nyumbani, itatusaidia sana kwenye malengo yetu kwani tukiwa tunahitaji ushindi mechi ya mwisho nyumbani, hatuwezi kushindwa," alisema Fadlu.

Katika mchezo huo, CS Constantine itaingia ikiwa inahitaji sare yoyote ili kuongoza Kundi A, kwani iko kileleni na pointi zake 12.

Simba, iliyo nafasi ya pili na pointi zake 10, inahitaji ushindi ili ifikishe pointi 13 na kuipiku CS Constantine ambayo kama itafungwa itasalia na pointi 12.

Iwapo timu hizo zitatoka sare, Constantine itaongoza kundi ikiwa na pointi 13 na Simba itamaliza ya pili ikiwa na pointi 11.

## Wachezaji Yanga

INATOKA UK. 24

mchezo kwa ushindi kwetu, hivyo baada ya hapa, tunageukia mchezo unaofuata ambao ni wa kufa ama kupona," alisema beki huyo anayemudu kucheza kati na pembeni kulia, ambaye alizungumza akiwa nchini humo.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema pamoja na ushindi huo hawawezi kuendelea kufurahia, badala yake kazi inahamia Dar es Salaam.

„Tuna mechi ya mwisho nyumbani, ni mechi muhimu sana kwa Yanga, tulikuwa na mechi ngumu, jasho limetuvuja kweli kweli, tumebakisha dakika 90 za moto ambazo zitamaliza mchezo wa Kundi A, na sisi tutakwenda robo fainali," alisema Kamwe.

Yanga na MC Alger zote zinawania nafasi moja, baada ya Al Hilal kufuzu ikiwa na pointi 10, ingawa bado haijawa na uhakika wa kumaliza ikiwa kinara wa kundi.

Yanga, iko nafasi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi saba, hivyo inahitaji ushindi pekee ili kufuzu, ambapo itafikisha pointi 10 na kuiacha MC Alger ikisalia na pointi zake nane.

Wakati huo huo, baadhi ya mashabiki wa MC Alger wameanza kutua nchini tayari kwa kuisapoti timu yao kwenye mchezo huo.

Kundi la kwanza la baadhi ya mashabiki wa timu hiyo limetua jana jijini Dar es Salaam, huku kundi lingine likitarajiwa kuwasili na timu.

MC Alger, yenye pointi nane kwenye nafasi ya pili, yenyewe inahitaji sare ya aina yoyote ili kufuzu kwani ikifanikiwa itakuwa imefikisha pointi tisa na Yanga itaambulia pointi nane pekee katika michezo sita ya hatua hiyo ya makundi.

Michezo
Jumatano Januari 15, 2025
Nipashe

Sababu CHAN kupigwa kalenda
UKURASA 20



# CAF yafungia mashabiki Simba, Fadlu afunguka

## ●●●Amwaga mbinu mbadala za kushinda mechi hiyo Jumapili nyumbani ambayo...

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF), limeifungia Klabu ya Simba kuingiza mashabiki kwenye mechi yao ya mwisho ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Constantine ya Algeria, unaotarajiwa kuchezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili wiki hii.

Kutokana na maamuzi hayo ya CAF, Klabu ya Simba imesitisha mauzo ya tiketi ya mchezo huo.

Taarifa kutoka CAF zilizotoka jana, zizothibitishwa na Klabu ya Simba jioni zinaeleza kuwa adhabu hiyo inatokana na vurugu zilizotokea kwenye mchezo wao dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia uliopigwa Desemba 15, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, uliomalizika kwa kupata ushindi wa mabao 2-1.

Taarifa iliyotolewa jana jioni na klabu hiyo ilisema imepokea maamuzi kutoka CAF kuhusu vurugu zilizojitokeza na kuifungia kwa michezo miwili.

"Hata hivyo, pamoja na kufungiwa michezo miwili, adhabu hiyo imepunguzwa na kuwa mchezo mmoja kucheza bila mashabiki pamoja na faini ya Dola za Kimarekani 40,000.

"Tunapenda kuufahamisha umma kuwa tunaendelea kufanya utaratibu ili kushughulikia uamuzi huo," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kutokana na adhabu hiyo ya CAF, klabu hiyo imetangaza kusitisha mauzo ya tiketi ya mchezo wa raundi ya sita ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Constantine.

"Kwa mashabiki ambao wameshanunua tiketi ni kwamba zitatumika kwenye mchezo ujao wa robo fainali. Klabu yetu itaendelea kusimamia taratibu, kanuni na sheria zinazozingatia usalama kwa jumla katika michezo," ilisema taarifa hiyo.

Vurugu zilitokea kwenye mchezo huo dakika za mwisho baada ya Kibu Denis kufunga bao la pili, ambapo baadhi ya viongozi, benchi la ufundi na wachezaji wa CS Sfaxien walivamia uwanja kutaka kumpiga mwamuzi kwa madai dakika zilikuwa zimemalizika, lakini jukwaani pia kulikuwa na vurumai kati ya mashabiki wa Simba na CS Sfaxien, ambapo vitu kadhaa viliripotiwa kung'olewa.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema tayari wamefahamu mfumo ambao wapinzani wao, CS Constantine, watacheza Jumapili ijayo, nao ni 'kupaki basi' ili kutafuta sare, hivyo kwa siku zilizobaki atazitumia kuwafundisha wachezaji wake jinsi ya kutegua mitego yao.

Fadlu alitoa siri hiyo baada ya kutua nchini alfajiri ya jana wakitoka Angola, ambako timu yake ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, ikilazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Bravos do Maquis, katika mchezo uliochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Novembro 11 jijini Luanda.

Alisema anachotaka kukifanya katika mchezo wa Jumapili ni kuutawala mchezo kwa asilimia nyingi, kuvunja mitego yote, kupasua ukuta waliouweka na mwishowe kuibuka na ushindi katika mchezo huo.

"Najua wanahitaji sare ili kuongoza kundi, kwa hiyo watakuja kucheza nyuma ya mpira, ka-

INAENDELEA UK. 23


Job

## Wachezaji Yanga watoa ahadi nzito

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA Msaidizi wa Yanga, Dickson Job, amebainisha kuwa yeye na wachezaji wenzake wamejipanga kucheza mchezo wa mwisho dhidi ya MC Alger ya Algeria kama hawatokuwa na mechi nyingine yoyote chini ya ardhi.

Yanga inatarajia kucheza mchezo wa mwisho wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, dhidi ya MC Alger, Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mpaka, Dar es Salaam.

Ni ushindi tu ndiyo utawafanya Mabingwa hao wa Tanzania Bara kufuzu hatua ya robo fainali kutoka Kundi A.

„Nimekaa na wachezaji wenzangu, tumeahidiana kuwa Jumamosi ndiyo siku ya kumaliza kazi, ndiyo fainali yetu, tumeapizana kwenda kucheza kama vile hatutokuwa na mchezo mwingine tena chini ya ardhi baada ya hapo. Yaani baada ya hapo hatutocheza tena. Maana yangu ni kwamba wachezaji tunatakiwa kujitoa bila kubakisha akiba ya chochote kile wala kujali lolote, nguvu, majeraha, kama hatutakuwa na mechi zingine mbele yetu," alisema Job.

Alisema iwapo watashindwa kufanya hivyo, basi hata mchezo wa Jumapili iliyopita ambao walishinda bao 1-0 dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, hautokuwa na maana yoyote.

Yanga ilishinda bao 1-0 ikiwa ugenini, Uwanja wa De la Capitale, jijini Nouakchott, nchini Mauritania, ambako timu hiyo inautumia kama uwanja wake wa nyumbani, kutokana na machafuko kisiasa kwao ya Sudan.

„Tulikuwa kwenye nafasi mbaya, tulizihitaji sana pointi hizi ili kuweza kujitengenezea mazingira mazuri ya kwenda robo fainali, sasa kama tumeshinda mchezo huu, haitokuwa na faida yoyote endapo hatutoshinda mchezo wa mwisho nyumbani, tulitaka kushinda huu ili tukamalizie

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >